DAUDI NA GOLIATI



NGUVU YA USHINDI DHIDI YA MAJITU KATIKA MAISHA YAKO

Mchungaji Christine Mlingi na Mlingi Elisha Mkucha

DAUDI NA GOLIATI

NGUVU YA USHINDI DHIDI YA MAJITU KATIKA MAISHA YAKO

DAUDI NA GOLIATI

NGUVU YA USHINDI DHIDI YA MAJITU KATIKA MAISHA YAKO

Kimeandikwa Na

Mchungaji Christine Mlingi
Mlingi Elisha Mkucha

Kimechapishwa Na

Havila Distributors Ltd
P. O. Box 16518
Dar es Salaam
Tanzania
Email: haviladl16@gmail.com
Tel: +255 713 227 037

Isipokuwa imeonyeshwa vinginevyo, nukuu zote za Maandiko zimechukuliwa kutoka Swahili Union Version

Nukuu ya maandiko iliyoonyeshwa [SUV] imechukuliwa kutoka Swahili Union Version: Hakimiliki – 1952, 1997: Chama cha Biblia Tanzania na Chama cha Biblia cha Kenya. Haki zote zimehifadhiwa.

Nukuu ya maandiko iliyoonyeshwa [NENO] imechukuliwa kutoka Kiswahili Contemporary Version (Neno: Biblia Takatifu): Hakimiliki – 1984, 1989, 2009, 2015 na Biblica, Inc. Haki zote zimehifadhiwa.

Nukuu ya maandiko iliyoonyeshwa [BHN] imechukuliwa kutoka Biblia Habari Njema kwa Watu Wote: Tafsiri ya Ushirikiano wa Makanisa (BHN): Hakimiliki – 1995, 2001: kwa Chama cha Biblia cha Tanzania na Chama cha Biblia cha Kenya. Haki zote zimehifadhiwa.

Daudi na Goliati – Nguvu ya Ushindi Dhidi ya Majitu katika Maisha Yako
Toleo la Kwanza.

ISBN 978-9976-88-278-0

Hakimiliki © 2020 na Christine Mlingi na Mlingi Elisha Mkucha
S.L.P. 1399
Dar ea Salaam
Tanzania

Kimechapishwa na:

Havila Distributors Ltd
S.L.P. 16518
Dar es Salaam
Tanzania
Email: haviladl16@gmail.com
Tel: +255 713 227 037

Kimechapishwa nchini Tanzania. Haki zote zimehifadhiwa chini ya Sheria ya Kimataifa ya Hakimiliki. Yaliyomo na / au ukurasa wa mbele au wa nyuma haviwezi kunakiliwa kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Waandishi.

ORODHA YA YALIYOMO

UTANGULIZI 1

SIKU YA KWANZA 5
SHETANI AMESHINDWA LAKINI BADO ANADHURU 5

SIKU YA PILI 12
HOFU LAZIMA ITOWEKE 12

SIKU YA TATU 16
PINGA NA KATAA ROHO YA KUKATALIWA. 16

SIKU YA NNE 20
ACHANA NA KUBWETEKA NA CHUKUA HATUA 20

SIKU YA TANO 26
LAZIMA TUITIISHE HASIRA 26

SIKU YA SITA. 31
URAIBU LAZIMA UTOWEKE 31

SIKU YA SABA 36
UPOFU LAZIMA UONDOKE. 36

SIKU YA NANE 43
TII AGANO LA MUNGU NA KUZIISHI AHADI ZAKE. 43

SIKU YA TISA 52
SONGA MBELE KWA USHINDI 52

HITIMISHO 57
MAOMBI YA VITA VYA KIROHO. 57
JINA NA DAMU YA YESU KAMA SILAHA YA VITA. 67
MAOMBI YA SIFA KWA MUNGU 74
MAOMBI YA MSAMAHA NA UREJESHO 76
ZABURI 91 SALA YA ULINZI. 79
SALA YA SHUKRANI. 82
MAOMBI YA KUMWABUDU NA KUMSUJUDU MUNGU. 84
ZABURI ZA KUSIMAMIA KATIKA MAOMBI 87

SHUKRANI. 89

UTANGULIZI

Mara nyingi sana tunafanya makosa makubwa katika suala la kuomba na kwa sababu hiyo imekuwa ngumu kupata majibu ya maombi yetu. Na pale tunapokosa kupata majibu ya maombi yetu tunakata tamaa na kupoteza kabisa tumaini letu kwa Yesu Kristo na hivyo kuanza kutafuta njia mbadala za kupata majibu ya changamoto tunazopitia. Hatimaye tunaishia kuwa watu wasio na imani na matumaini kwa Mungu, tunaweka imani zetu kwa watu na vitu na hivyo kumfanya Mungu ageuze kabisa uso wake kinyume yetu.

Cha msingi sana kuzingatia ni wewe binafsi kufuata maelekezo ambayo Mungu ametupatia kupitia Neno lake kwani Biblia inasema, ***"Amin, nawaambia, YEYOTE atakayeuambia mlima huu, ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake. Kwa sababu hiyo nawaambia, yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu."*** (Marko 11:23)

Kwa hiyo tatizo liko kwetu na siyo kwa Mungu katika kupokea majibu ya maombi yetu. ***"Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu: OMBENI, NANYI MTAPATA; furaha yenu iwe timilifu"*** (Yohana 16:24). Na mtu asipojibiwa maombi yake anaanza kutangatanga, mara leo yuko huku, mara kesho kule, unakuwa mtoto asiyekuwa na mzazi wa kudumu, hatimaye unaangukia kwenye mikono isiyokuwa salama na kufilisiwa kabisa. Unapaswa kutuliza akili yako, uutafute uso wa Mungu kwa bidii nawe utapata majibu ya maombi yako. Yeremia 29:11-13 inasema "*Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema BWANA, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho. Nanyi mtaniita, mtakwenda na kuniomba, nami nitawasikiliza.* ***Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote."***

Biblia inasema, ***"Niite nami nitakuitikia ...."*** (Yeremia 33:3), na haijasema niite nami nitakunyamazia. Aidha Methali 8:17 inasema ***"Nawapenda wale wanipendao, Na wale wanitafutao kwa bidii wataniona."*** Biblia haijasema ukimpenda Mungu atakuchukia au ukimtafuta kwa bidii hataonekana kwako au atakaa kimya. Amesema utamuona. Hivyo, katika maombi pia jifunze sana kusoma na kusimama na Neno la Mungu maana ndilo litakalokupatia njia ya kumfikia Mungu kama Yakobo 4:8 inavyosema, ***"Mkaribieni Mungu, naye***

atawakaribia ninyi. Itakaseni mikono yenu, enyi wenye dhambi, na kuisafisha mioyo yenu, enyi wenye nia mbili."

Ukifanya hivyo, utapata kibali cha kujibiwa maombi yako na Mungu. Ebu jifunze kitu katika mazungumzo haya kati ya Musa na Mungu katika Kutoka 33:12-16;

> ***"Musa akamwambia Bwana, Angalia, wewe waniambia, Wachukue watu hawa; nawe hukunijulisha ni nani utakayemtuma pamoja nami. Walakini umesema, Nakujua jina lako, nawe umepata neema mbele zangu. Basi, sasa nakuomba, ikiwa nimepata neema mbele zako, unionyeshe njia zako, nipate kukujua, ili nipate neema mbele zako; ukakumbuke ya kuwa taifa hilo ndilo watu wako. Akasema, Uso wangu utakwenda pamoja nawe, nami nitakupa raha. Naye akamwambia, Uso wako usipokwenda pamoja nami, usituchukue kutoka hapa. Kwa maana itajulikanaje kuwa nimepata neema mbele zako, mimi na watu wako? Siyo kwa sababu unakwenda pamoja nasi, hata mimi na watu wako tutengwe na watu wote walio juu ya uso wa nchi?"***

Musa alitambua kuwa bila Mungu kuwa pamoja na wana wa Israeli katika safari ya kutoka Misri kwenda Kanani basi wasingeweza kushinda changamoto na vikwazo vingi ambavyo wangekutana navyo. Hivyo, Musa akamsihi Mungu kwamba awe nao katika safari hiyo na Mungu akamuahidi Musa kwamba ***"Uso wangu utakwenda pamoja nawe, nami nitakupa raha"*** (Kutoka 33:14).

MATHAYO 28:20 (SUV)

"...NA TAZAMA, MIMI NITAKUWA PAMOJA NANYI SIKU ZOTE, HATA UKAMILIFU WA DAHARI"

Kwa namna hiyo hiyo, Yesu ametuahidi kutokutuacha kamwe na kwamba atakuwa pamoja nasi hata ukamilifu wa dahari (Mathayo 28:20). Haijalishi unapitia changamoto na vikwazo vya aina gani katika maisha yako kiasi cha kukata tamaa kabisa na kuhisi umefikia mwisho wa maisha au hatma yako. Yesu aliyekiacha kiti chake cha enzi mbinguni kuja kufa kwa ajili yako msalabani, akashinda kifo na mauti na kufufuka, yeye anakupa uzima tele. Simama juu kwa miguu yako uvikwe nguvu mpya na uchukue hatua kama vile Daudi alivyochukua hatua katika mazingira ambayo jeshi la Israeli na mfalme wao Sauli walikuwa wamekata tamaa kabisa, lakini yeye akasimama, akampiga na kumuua Goliati.

Hivyo, katika kitabu hiki tutajifunza siri ya ushindi wa kiroho katika changamoto mbalimbali tulizonazo katika maisha yetu ya kila siku kupitia kisa cha Daudi na Goliati. Ndani ya siku nane, utajifunza siri za ushindi alizotumia Daudi kumshinda Goliati na kupitia siri hizo, utaweza pia kupata ushindi mkubwa kwa kila changamoto unayoipita.

Aidha, utapata maandiko ya Neno la Mungu ya kusimama nayo katika maombi na kisha utapata muhtasari wa maombi unayopaswa kuomba katika kila eneo. Hatimaye kwenye hitimisho tumekuandalia mafunzo yatakayokupa msingi wa namna ya kuomba maombi ya vita yatakayokupa ushindi kwa kila vita unayopitia. Katika eneo hili tumekuandalia pia maombi ya sifa, kuabudu na kushukuru; toba, ulinzi, kuangamiza na kuteketeza nguvu za giza kwa uweza na nguvu ya damu ya Yesu.

Naamini ukisoma na kuweka katika matendo yote yaliyomo katika kitabu hiki utaishi maisha ya ushindi na kupata majibu sahihi kwa yote unayoyaomba kwa Mungu kupitia Jina la Yesu Kristo. Jitahidi sana kila siku, katika siku nane, kusoma maandiko yaliyoainishwa kwa siku hiyo na kufanya maombi ya siku hiyo na yale yaliyoko katika Hitimisho na utaanza kuona mabadiliko halisi katika maisha yako ya wokovu.

3 YOHANA 1:2 (SUV)

MPENZI NAOMBA UFANIKIWE KATIKA MAMBO YOTE NA KUWA NA AFYA YAKO, KAMA VILE ROHO YAKO IFANIKIWAVYO.

Mungu akubariki sana unapochukua hatua ya kuishi maisha ya ushindi, yatakayokupa ushuhuda mkubwa. Nami nakuombea Mungu akufanikishe katika yote uyaombayo na hasa pale unapochukua hatua ya kuishi maisha ya utakatifu, kwa sababu, kwa kufanya hivyo, ndivyo pia utafanikiwa katika mambo yote na kuwa na afya njema (3 Yohana 1:2).

Daima kumbuka; Ikiwa Mungu alifunga makanywa ya simba ili wasimdhuru Daniel; akawa mtu wa nne katika tanuru la moto walimoingizwa Shadraki, Meshaki na Abednego ili wasidhurike na moto huo; akaigawanya bahari ya Shamu kwa ajili ya Musa na wana wa Israeli na kuwafanya

MWANZO 18:14 (SUV)

KUNA NENO GANI LILILO GUMU LA MSHINDA BWANA ? KWA MUHULA WAKE NITAKURUDIA, WAKATI HUU HUU MWAKANI, NA SARA ATAPATA MWANA WA KIUME.

WAEFESO 3:20 (SUV)

BASI ATUKUZWE YEYE AWEZAYE KUFANYA MAMBO YA AJABU MNO KULIKO YOTE TUYAOMBAYO AU TUYAWAZAYO, KWA KADIRI YA NGUVU ITENDAYO KAZI NDANI YETU.

wapite ikiwa kama nchi kavu; akalifanya jua kusimama kwa ajili ya Yoshua; akaifungua jela kwa ajili ya Petro; akamfanya Sara apate uzazi hali alikuwa ni tasa; na akamfufua Lazaro kutoka wafu; basi kwa kadri hiyo hiyo anaweza hakika kukutendea mema! Hakuna lolote unalokabiliwa nalo leo ambalo ni gumu la kumshinda Mungu (Mwanzo 18:14). Kitu cha muhimu ni kuhakikisha unayo nguvu ya kutosha ya Mungu ndani yako kwa sababu, kwa kadri ya nguvu hiyo ndivyo pia Mungu anajibu na kutenda zaidi ya vile tuombavyo au tuwazavyo (Waefeso 3:20).

SIKU YA KWANZA

SHETANI AMESHINDWA LAKINI BADO ANADHURU

Kisa cha Biblia cha Daudi na Goliati kinafahamika sana na wangu wengi. Upande mmoja wa bonde la Ela lilikuwepo jeshi la Wafilisti na shujaa wao aliyeitwa Goliati. Upande mwingine wa bonde hilo lilikuwepo jeshi la Waisraeli, waliojawa na woga na hofu kubwa wakiongozwa na Mfalme Sauli. Kwa siku arobaini Goliati alikuwa akiwadhihaki Waisraeli na kuwajaza hofu kubwa. Kila siku alikuwa akiwataka kumtuma shujaa wao mmoja ili apigane naye na atakayeshinda mwenziwe basi jeshi lake litakuwa limeshinda vita hivyo. Hata hivyo, Waisraeli walishindwa kumpeleka mmoja wao kupigana na Goliati.

Inawezekana maisha yako yanafanana kabisa na kisa hiki walichokutana nacho Waisraeli. Labda kuna aina fulani ya jitu lililosimama mbele yako likikudharau, kukusumbua na kukutukana. Labda ni hofu. Labda ni hasira. Labda unajisikia kukataliwa. Labda ni ugonjwa sugu. Labda ni kuathirika kwa madawa ya kulevya, uasherati, uzinzi, ulevi n.k.

Haijalishi ni jitu gani linalokabili maisha yako, ambalo siku hadi siku limekuwa likikusonga. Umejaribu mara nyingi kwa nguvu zako mwenyewe kukabiliana na manyanyaso hayo bila kufanikiwa. Umeshindwa kusonga mbele. Hatimaye unaona wazi kabisa unashindwa kuishi maisha yenye uhuru kamili ambayo Mungu anataka uyaishi.

Habari njema ni kwamba Mungu amefanya njia ya majitu hayo kuanguka. Inaanza kwa wewe kuamini kwamba pamoja na kwamba majitu hayo unayopambana

WAEFESO 6:10-18

HATIMAYE MZIDI KUWA HODARI KATIKA BWANA NA KATIKA UWEZA WA NGUVU ZAKE. VAENI SILAHA ZOTE ZA MUNGU, MPATE KUWEZA KUZIPINGA HILA ZA SHETANI. KWA MAANA KUSHINDANA KWETU SISI SI JUU YA DAMU NA NYAMA; BALI NI JUU YA FALME NA MAMLAKA, JUU YA WAKUU WA GIZA HILI, JUU YA MAJESHI YA PEPO WABAYA KATIKA ULIMWENGU WA ROHO. KWA SABABU HIYO TWAENI SILAHA ZOTE ZA MUNGU, MPATE KUWEZA KUSHINDANA SIKU YA UOVU, NA MKIISHA KUYATIMIZA YOTE, KUSIMAMA. BASI SIMAMENI, HALI MMEJIFUNGA KWELI VIUNONI, NA KUVAA DIRII YA HAKI KIFUANI, NA KUFUNGIWA MIGUU UTAYARI TUPATAO KWA INJILI YA AMANI; ZAIDI YA YOTE MKIITWAA NGAO YA IMANI, AMBAYO KWA HIYO MTAWEZA KUIZIMA MISHALE YOTE YENYE MOTO YA YULE MWOVU. TENA IPOKEENI CHAPEO YA WOKOVU, NA UPANGA WA ROHO AMBAO NI NENO LA MUNGU; KWA SALA ZOTE NA MAOMBI MKISALI KILA WAKATI KATIKA ROHO, MKIKESHA KWA JAMBO HILO NA KUDUMU KATIKA KUWAOMBEA WATAKATIFU WOTE.

nayo ni makubwa, lakini si makubwa kumshinda Yesu Kristo. Kwa uhakika tayari Yesu amekwisha yashinda pale msalabani ili uishi maisha ya ushindi. Alipokuja hapa duniani, aliteswa, akafa, akazikwa na hatimaye akafufuka ili wewe uweze kuishi maisha ya ushindi. Alikuja kukuweka huru dhidi ya majitu yanayoinuka dhidi yako na kukufanya uishi maisha ya kuteseka na kwa hofu.

Yesu amekwisha mshinda adui. Hata hivyo, kama tunavyosoma katika 1 Petro 5:8 ***".....mshitaki wenu Ibilisi, kama simba aungurumaye, huzungukazunguka, akitafuta mtu ammeze."*** Kwa namna nyingine, ni kama nyoka ambaye kichwa chake kimekatwa. Unapomuua nyoka hakikisha umezika kichwa chake, kwa sababu hata baada ya kumuua bado nyoka anakuwa na sumu kali katika meno yake. Ukikanyaga kwenye kichwa cha nyoka aliyekufa, bado unaweza kuathiriwa na sumu yake. Kwa namna hiyo hiyo, hata kama Yesu Kristo alikwisha vunja nguvu za shetani pale msalabani, bado shetani anaweza kutuathiri kwa sumu yake kali. Amekwisha shindwa lakini bado sumu yake ni hatari.

Lengo basi ni kutokukanyaga kwenye kichwa cha nyoka. Kwa maana nyingine, ni wajibu wetu kumtii Mungu na kumpinga shetani, naye atatukimbia (Yakobo 4:7), kwa kutumia silaha za vita

YAKOBO 4:7 (SUV)

BASI MTIINI MUNGU. MPINGENI SHETANI, NAYE ATAWAKIMBIA

ambazo Yesu ametupatia (Waefeso 6:10-18), na kujiegemeza katika utoshelevu wake (Mithali 3:5, 6). Inapaswa ukumbuke kuwa Yesu ndiye Daudi wako katika simulizi hii – kwamba huwezi kamwe kuyashinda hayo majitu kwa ujasiri wako, nguvu zako au juhudi zako. Siku zote ni Yesu anayeyashinda majitu yanayokusonga katika maisha yako.

MITHALI 3:5-6

MTUMAINI BWANA KWA MOYO WAKO WOTE, WALA USIZITEGEMEE AKILI ZAKO MWENYEWE; KATIKA NJIA ZAKO ZOTE MKIRI YEYE, NAYE ATAYANYOSHA MAPITO YAKO

Kama kweli unataka kuona ushindi dhidi ya majitu yanayokusonga katika maisha yako, unapaswa kutambua utegemezi wako juu ya ukamilifu wote wa Yesu Kristo. Ushindi wako unatokana na kumtegemea Yesu Kristo na hautokani na kujitahidi kwako kufanikiwa, kama ilivyoandikwa katika Zaburi 64:2 ***"utanificha mbali na shauri la siri la watenda mabaya, mbali na ghasia ya watu wafanyao maovu."*** Hivyo basi, hatua ya kwanza ya kuchukua dhidi ya adui yako ambaye tayari ameshindwa lakini bado ana sumu kali, ni kufanya mabadiliko ya mawazo katika akili yako kwamba hakuna jambo lolote linalomshinda Mungu na kwamba wewe ni mshindi katika Yesu Kristo (Yeremia 32:27). Kristo ndiye nguvu pekee inayoleta mabadiliko ya kweli katika maisha yako na kukupa ushindi dhidi ya kila aina ya majitu unayopambana nayo.

YEREMIA 32:27

TAZAMA, MIMI NI BWANA, MUNGU WA WOTE WENYE MWILI; JE! KUNA NENO GUMU LOLOTE NISILOLIWEZA?

Katika simulizi hii ya Daudi na Goliati, utagundua kwamba Daudi alitambua wazi kuwa uweza wa ushindi wake ulikuwa nje ya nguvu zake binafsi au uwezo wa silaha za kivita walizokuwa nazo wana wa Israeli. Maandiko yanasema: ***"Ndipo Daudi akamwambia yule Mfilisti, Wewe unanijia mimi na upanga, na fumo, na mkuki, bali mimi ninakujia wewe kwa jina la Bwana wa majeshi, Mungu wa majeshi ya Israeli uliowatukana "*** (1 Samweli 17:45).

Maneno haya yenye nguvu aliyoyatamka Daudi yanaonyesha wazi kwamba Daudi alitambua uweza ulio ndani ya Jina la Bwana Mungu aliye hai ni zaidi ya silaha zote za adui. Kwa maana hilo Jina la Bwana Mungu wetu lililo hai lina utiisho usioweza kuelezeka wala kutafsirika kwani Goliati hakuwa na hofu ya aina yoyote ya silaha waliyokuwa nayo wana wa Israeli wala kumuogopa kiumbe kingine chochote kile. Alijiona yeye hawezi kushindwa na chochote na kwamba alikuwa

daima ni mshindi wakati wote.

Hivi ndivyo alivyo adui yako mbele zako. Wakati wote anapokuja kwako hujiona ni bora na mshindi. Huja na vitisho vikubwa na mara zote vile vitisho ndivyo hukukatisha tamaa na kukuvunja moyo na kukufanya ushindwe vita hata kabla ya kuingia kwenye vita yenyewe.

Napenda kukutia moyo ndugu msomaji kwamba Daudi asingeweza kumshinda Goliati wa Gathi kwa kutumia upanga, fumo wala mkuki. Laiti kama Daudi angelimwendea Goliati kwa silaha za mwili basi ni dhahiri kabisa angelipigwa hadi kufa na mwili wake ungelikuwa chakula cha ndege. Ila Daudi alimwendea Goliati kwa uweza wa Jina la Bwana Mungu aliye hai na hatimaye alipata ushindi.

Ukisoma maandiko katika 1 Samueli 17:38-39 utamuona Sauli akimvika Daudi mavazi ya vita. Sauli alitambua kuwa ushindi wa Daudi unaweza kupatikana kupitia silaha za mwili, ila Daudi alipoyajaribu mavazi yale alitambua kuwa vita anavyokwenda kupigana wala havihitaji silaha za mwili bali zile zilizo na uwezo katika Bwana.

Daudi akazivua silaha alizovikwa na Sauli na kuziweka chini na akavaa silaha za rohoni. Angalia jinsi Daudi anavyosema: ***"Nao jamii ya watu wote pia wajue ya kwamba Bwana haokoi kwa upanga wala kwa mkuki; maana vita ni vya Bwana, naye atawatia ninyi mikononi mwetu"*** (1 Samweli 17: 47).

Ni mara nyingi tunafanya makosa katika vita vya kiroho. Tunatamani sana kupigana vita kabla ya kuelewa ni aina gani ya vita tunayopigana. Daudi anatufundisha somo zuri sana la umuhimu wa kutambua aina ya vita inayosimama mbele yako kama Goliathi wako na aina ya silaha za kutumia ili uweze kumshinda. Mara nyingi tumekuwa tukisema vita si yetu bali ni ya Bwana. Msemo huu umezoeleka sana kwa wakristo na ni wengi wetu tumekuwa tunautumia, lakini kutendea kazi kile tunachokisema imekuwa changamoto kwani mara nyingi tunatamka pasipo kuelewa vizuri maana halisi ya tamko hili.

Tambua kwamba Sauli hakujua siri ya ushindi dhidi ya Goliati. Yeye pamoja na jeshi lote la Israeli walidhani kuwa ushindi unapatikana kwa kutumia upanga na mkuki ndio maana Sauli alimvalisha Daudi silaha zake za kivita. Daudi aliyejua siri hii alikataa hizo silaha za vita ya mwili akakumbuka kuwa msituni alipokua akichunga kondoo, simba na dubu walipotaka kuvamia kondoo, yeye alipata

ushindi bila hata kutumia panga na mikuki, hata hivyo alishinda kwa kuwaua simba na dubu.

Imani hii ilimtia moyo na mara moja aliuona ushindi wa kumuangamiza adui yao kabla hata hajamfikia. Katika vita lazima tujifunze sana imani, kujiamini, kujikubali na kuyakumbuka mahusiano yako na Mungu yakoje! Hili ni jambo la msingi sana katika vita vya kiroho ili uweze kumshinda adui yako.

Simulizi hii inatufundisha pia kwamba hakuna ushindi pasipokuwepo na vita. Au kwa maneno mengine, huwezi kupiga hatua kubwa katika maisha yako na kufikia mafanikio makubwa bila kupigana na kushinda vita. Daudi asingekuwa mshindi kama vita isingelikuwepo, au kwa lugha nyingine ni kwamba Daudi asingelipata ushindi pasipo kuwepo dubu, simba na Goliati. Hivyo Goliati alihitajika kuwa kisababisho kikuu cha ushindi wa Daudi. Kama ni hivyo basi, Goliati ni muhimu maishani mwetu kwani hatuwezi kufikia mafanikio bila vita.

Mara zote unapaswa kutambua kwamba vita yako ndio inayokutambulisha wewe ni nani na pia ukubwa wa vita yako ndio unaoakisi ukubwa wa ukuu wako. Huwezi kuwa na vita ndogo halafu utarajie kuinuliwa kwa kiwango kikubwa. Ni ukweli usiopingika kwamba, pamoja na kwamba Daudi alikwisha pakwa mafuta kuwa mfalme wa Israeli, lakini alitakiwa kushindana na ufalme ili hatimaye aweze kukalia kiti cha kifalme. Hivyo, ushindi wa Daudi dhidi ya Goliati ndio uliosherehesha ufalme wake. Ebu angalia namna maandiko yanavyosema katika 1 Samweli 18:6-9;

> ***"Hata ikawa, walipokuwa wakienda, hapo Daudi aliporudi baada ya kumwua yule Mfilisti, wanawake wakatoka katika miji yote ya Israeli, kwa kuimba na kucheza, ili kumlaki mfalme Sauli; wakatoka na matari, na shangwe, na vinanda. Nao wale wanawake wakaitikia wakicheza, wakasema,***
>
> ***Sauli amewaua elfu zake, na Daudi makumi elfu yake.***
>
> ***Basi Sauli akaghadhibika sana, na maneno haya yakamchukiza; akasema, Wamempa Daudi makumi elfu, na mimi wamenipa elfu tu; kuna nini tena awezayo kupata, isipokuwa ni ufalme?"***

Ushindi wa Daudi dhidi ya Goliati ukamfanya ghafla kuwa shujaa na kutambulika

katika Israeli nzima. Kabla ya hapo, hakuna aliyetambua ushindi wake dhidi ya simba na dubu. Ilimpasa Daudi akutane na vita kubwa zaidi ya hiyo na kuishinda ili aweze kutambulika katika Israeli nzima na hivyo kufikia hatma ya kuwa mfalme wa Israeli.

Unapaswa kutambua kuwa ili umshinde adui yako, ni lazima umshinde kiroho kwanza. Jambo lolote linalotokea chini ya jua, ujue limeshatokea katika ulimwengu wa roho. Vita dhidi ya Daudi na Goliati ilianza kupiganwa katika ulimwengu wa roho, ndio maana tunaona Goliati akimkabidhi Daudi katika mikono ya miungu yake, naye Daudi akimkabidhi Goliati kwa MUNGU Mkuu.

Mkristo anayepambana vizuri kiroho hata jaribu lije baadaye uwe na uhakika kwamba atalishinda hilo jaribu kwa sababu alikwisha zoea kupambana kabla ya vita haijamjia. Leo hii, Goliati bado yupo, lakini ukihitaji kumshinda, wewe muendee kwa Jina la Bwana Mungu wa Majeshi. Tuna ushindi mkubwa kwa sababu sisi ni Daudi wa leo.

Mtoto wa Mungu, unapaswa kutambua kwamba dubu, simba na Goliati wako anaweza kuwa hata ndugu zako, rafiki zako, wafanyakazi wenzako au mkubwa wako kazini ambao wanakufuatilia kwa ubaya hata kukudhihaki. Ajapokudharau, wewe usimdharau. Ajapokusema ovyo, wewe kaa kimya. Ajapokuinukia, wewe usimwinukie kwa maneno wala kupigana naye, bali muone mtu huyo ni kama Goliati kwa Daudi.

Wewe usishindane naye, kwani huwezi wewe kumshinda Goliati kwa maneno. Daudi alisema hivi katika 1 Samweli 17:32 "***...Asizimie moyo mtu yeyote kwa ajili ya huyu; mimi mtumishi wako nitakwenda kupigana na Mfilisti huyu."*** Maneno haya yalikua ni ya kishujaa sana. Na ndivyo jeshi la Bwana linavyotakiwa kuwa. Kwa sababu Bwana tuliye naye ni shujaa wa vita; jeshi ambalo ni imara tayari kupigana vita vizuri vya kiroho kwa ushindi mkuu, huwa imara siku zote kama Daudi.

ANDIKO LA KUSIMAMIA

1 Petro 5:8-9
Yeremia 32:27

MAOMBI

Baba, naomba unipe ufahamu zaidi kuhusu tumaini la mwito wangu na lile unalotaka mimi nitekeleze katika maisha yangu ya kiroho. Naomba kila siku nifunikwe na silaha ya kiroho ya Mungu, ambayo umetoa kwa watoto wako wote, kujua kwamba vita vyetu si vita vya damu na nyama bali ni juu ya falme na mamlaka na nguvu zote za uovu.

Nisaidie nijikaze viuno vya akili yangu kwa injili ya kweli, na kwa dirii ya kweli kifuani ili niweze kutembea kwa amani yako toshelevu. Nisaidie kudumisha imani yangu kwako na kulinda moyo na nia yangu kwa wokovu kupitia Yesu Kristo.
Niimarishe kwa upanga wa roho, ambao ni neno la Mungu, ili niweze kujilinda dhidi ya mafundisho ya udanganyifu na mafundisho ya mashetani yanayopotosha wengi. Niwezeshe kusimama imara katika Kristo, kujua kwamba ni katika Wewe pekee ndipo ulipo ushindi wangu dhidi ya dunia, mwili na shetani na hivyo nitasimama nikiwa salama.

SIKU YA PILI

HOFU LAZIMA ITOWEKE

Unaposoma simulizi ya Daudi na Goliati katika Biblia, moja ya kitu cha kwanza kabisa unachokutana nacho ni kwamba jeshi la Waisraeli lilikuwa limekata tamaa na kushikwa na hofu kubwa dhidi ya lile jitu Goliati (1Samuel 17:11). Kila siku Goliati alianza kwa kulidhihaki jeshi la Waisraeli. Kadri siku zilivyopita ndivyo jeshi la Waisraeli lilivyozidi kuvunjika moyo na kukata tamaa. Walianza kuamini kwamba jambo baya lingeweza kuwatokea ... kushindwa vita.

1 SAMUEL 17:11

BASI SAULI NA ISRAELI WOTE WALIPOSIKIA MANENO HAYO YA MFILISTI, WAKAFADHAIKA NA KUOGOPA SANA

Kwa ufupi, hii ndiyo maana ya hofu – kuamini kwamba kuna jambo baya linakwenda kukutokea ambalo huna namna ya kulizuia. Hofu hii inaweza kujidhihirisha kwa namna tofauti - wasiwasi, woga, shida, kukata tamaa, msongo wa mawazo, n.k. na inaweza kusababishwa na mambo mbalimbali. Labda unakutana na hofu kutokana na mazingira uliyokulia. Labda familia yako iliyachukulia maisha kama jambo lenye kuogofya sana. Kwamba, muda wowote jambo lolote baya linaweza kutokea.

Kwa mfano, kuna baadhi ya jamii, hasa maeneo ya vijijini, kufanya jambo la kimaendeleo kama vile kujenga nyumba ya kisasa, kuanzisha biashara kubwa n.k. ni jambo la kuogofya kwa sababu, kihistoria, watu waliojaribu kufanya hivyo walifariki kwa njia zinazoaminika kuwa ni za kishirikina au kichawi. Hivyo jamii hizo zinaendelea kuwa katika hali duni ya kimaisha na kimaendeleo. Watu kutoka

katika jamii hizo wanaojaliwa kupata kipato cha kuwawezesha kufungua miradi ya kimaendeleo wanalazimika kufanya hivyo mbali na maeneo yao ya asili.

Inawezekana pia unapata hofu kwa sababu ya jitihada zako za kuficha makosa na mapungufu katika maisha yako. Unaona aibu ya jambo ulilowahi kufanya siku za nyuma na una woga kwamba litakuja kufahamika na kuwa wazi mbele ya jamii. Au labda unaona hofu kwa kujaribu kudhibiti vitu vingi sana katika maisha yako kwa wakati mmoja. Umegundua kuwa vitu vingi katika maisha yako huwezi tena kuvidhibiti na hilo linakupa hofu kubwa kuhusu hatima yake kwako hapo baadaye.

Hilo jitu la hofu linaweza kuweka mizizi ndani ya maisha yako na kuanza kukutawala. Linaweza kukukatisha tamaa na hatimaye kufifisha utukufu wa Mungu katika maisha yako. Linaweza kutafuna maisha yako, kuharibu hisia yako ya kujiamini, kukuibia usingizi, kukupofusha, na kukuibia sifa yako kwa Mungu. Hofu ni jitu kubwa na ni lazima lianguke kwa nguvu ya Jina la Yesu Kristo.

MATHAYO 19:26

YESU AKAWAKAZIA MACHO, AKAWAAMBIA, KWA WANADAMU HILO HALIWEZEKANI; BALI KWA MUNGU YOTE YANAWEZEKANA.

Suluhisho la kupambana na jitu hofu siyo uamuzi bali ni imani katika Yesu Kristo. Siyo tu kusema "hofu ondoka" lakini kukiri "Nina imani kwamba Yesu ni mkubwa zaidi kuliko hili jitu hofu na tayari amekwisha lishinda." Katika Warumi 10 :17 Paulo anasema ***"Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo."*** Unapoona na kumsikia Mungu ndani yako na kupitia Neno lake, Neno linakuruhusu kuona na kusikia kwamba yeye Mungu ni mkuu kuliko majitu yote unayopitia katika maisha yako. Hilo linajenga imani yako, na imani yako inafanyika jiwe la kulipiga lile jitu ambalo tayari limekwisha shindwa.

Kwa hiyo, leo tambua chanzo cha hofu yako na kiweke katika mikono ya Yesu. Zaburi 34:4 inasema, ***"Nalimtafuta BWANA akanijibu, Akaniponya na hofu zangu zote."*** Jikumbushe kuwa kwa Mungu mambo yote yanawezekana (Mathayo 19:26) na ana uwezo wa kulishinda hilo jitu. Kumbuka kwamba Yesu ameahidi daima kuwa nawe (Waebrania

1 PETRO 5:7

HUKU MKIMTWIKA YEYE FADHAA ZENU ZOTE, KWA MAANA YEYE HUJISHUGHULISHA SANA KWA MAMBO YENU

13:5). Taja kila kitu kinachokukosesha usingizi na yaweke hayo madhila yote kwake yeye aliyekwisha kuahidi kujitwika fadhaa zako zote (1 Petro 5:7). Kumbuka Yesu alitupenda na kutufia msalabani ili kuchukua mizigo yetu na katika pendo lake hakuna hofu (1Yohana 4:18). Baada ya hapo jaza kimya chako na sifa kwa sababu unaona na kukiri nguvu za Mungu, unatambua upendo wake kwako, na unajua daima atakushindia. Rehema zake hazitashindwa kamwe (Maombolezo 3:22, 23).

Unapofanya hivi, hata kama chanzo cha hofu yako kinapokuwa hakijatoweka bado, kwa ukamilifu kabisa utakuwa umeirudisha hofu mahali pake panapostahili: katika mikono salama ya Yesu Kristo.

1 YOHANA 4:18

KATIKA PENDO HAMNA HOFU; LAKINI PENDO LILILO KAMILI HUITUPA NJE HOFU, KWA MAANA HOFU INA ADHABU; NA MWENYE HOFU HAKUKAMILISHWA KATIKA PENDO

ANDIKO LA KUSIMAMIA

Isaya 43:1, 2
Mithali 3:24-26

MAOMBI

Mungu Baba, Yesu ambaye ni Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu, naja kwako leo, nikiwa nahitaji ukombozi wako kutoka katika roho ya hofu! Roho hii ya hofu inaninyemelea kila siku na kujaribu kuniondoa kutoka katika njia inipasayo ya mafanikio yangu. Roho hii inaniambia kwamba kila jambo langu halitafanikiwa na kila kitu nilichonacho kitasambaratika na kwamba hakuna matumaini yoyote.

Lakini leo, nachagua kukumbuka na kutambua kwamba MIMI NI MKRISTO Nimeteuliwa na Mungu kama mzao wake mteule, taifa takatifu (1 Petro 2:9) Nimesamehewa dhambi zangu zote, si tu baadhi, bali dhambi zangu zote Nimekombolewa na kuhamishwa kutoka katika ufalme wa giza kwenda katika ufalme wa nuru wa Mungu kupitia Yesu Kristo (Matendo 26 :18) Mimi ni mali ya Mungu na hakuna awaye yeyote anayeweza kuniondoa katika mikono yake (Yohana 10:28-29)

Nimepewa mamlaka dhidi ya shetani na kazi zake zote (ikiwa ni pamoja na roho

ya hofu). Luka 10:19

Mungu hajanipa roho ya hofu, bali ya NGUVU, UPENDO na MOYO WA KIASI (2 Timotheo 1:7). Kwa hiyo, kwa Jina, Uwezo na Mamlaka ya Yesu Kristo Mwana wa Mungu, nakuomba Roho Mtakatifu, ufunge roho yoyote ile ya hofu inayojaribu kufanya kazi katika maisha yangu. Funga kila roho chafu inayojaribu kufanya kazi katika maisha yangu, na naikaripia, kuiondoa na kuifuta kabisa katika maisha yangu.
Naikaripia iondoke kutoka katika nyumba yangu
Naikaripia iondoke kutoka maisha yangu (Marko 4:39)
Kwa Jina, Uweza na Mamlaka ya Yesu Kristo, BWANA na MWOKOZI wangu
Naikaripia sasa, na nachagua IMANI kupitia Jina la Yesu Kristo.

Nachagua na kutambua Mungu hana makusudi ya kuachilia mambo mabaya yatokee katika maisha yangu, badala yake Mungu ndiye msaada wangu aninyanyuaye kila mara niangukapo, ili kwamba niendelee mbele, kwa mamlaka ya Jina lake Takatifu.

Yesu Kristo, Nimekupa moyo wangu, kwa hiyo nakupa pia maisha yangu, mwili wangu na akili yangu.
Nahitaji msaada wako
Tafadhali, nitie nguvu ya kushinda
Nakuhitaji BWANA Yesu
Nachagua kukutegemea wewe sasa, na nakuomba kwamba lolote lile mimi na familia yangu tunalopitia basi ukabiliane nalo wewe na naliacha katika mikono yako salama.

Nisaidie BWANA wangu
Nisaidie kutambua kwamba umeachilia katika maisha yangu maisha ya ushindi na kwamba Mimi ni mshindi na zaidi ya kushinda kupitia wewe Yesu Kristo unayenipenda (Warumi 8:37)

Nilinde BWANA wangu ili niridhike kwa vitu ulivyoviachilia katika maisha yangu kwa sababu wewe mwenyewe umeniambia sitakupungukia wala sitakuacha kabisa, nami sitaogopa, mwanadamu atanitenda nini? (Waebrania 13:5-6).

Ninaomba hayo yote na kuamini kupitia Jina la BWANA wangu Yesu Kristo, Amen.

SIKU YA TATU

PINGA NA KATAA ROHO YA KUKATALIWA

Daudi alikuwa kijana mdogo sana alipofika eneo la vita kati ya Waisraeli na Wafilisti. Hakuwa mwanajeshi, bali alifika ili kuwaletea chakula ndugu zake. Alipofika kwenye kambi ya jeshi la Waisraeli, alimsikia Goliati akiwadhihaki Waisraeli na kuwauliza nani kati yao angeweza kupigana naye. Ndugu zake hawakufurahishwa na maswali yake ya uchunguzi. Angalia neno hili, ***"Naye Eliabu, mkubwa wake, alisikia hapo alipoongea na watu; na hasira yake Eliabu ikawaka juu ya Daudi, akasema, Mbona wewe umeshuka hapa? Na kondoo wale wachache umemwachia nani kule nyikani? Mimi nakujua kiburi chako, na ubaya wa moyo wako; maana umeshuka ili upate kuvitazama vita."*** (1 Samuel 17:28).

Maneno haya hayashangazi kama tunaelewa simulizi nzima. Katika 1 Samuel 16, tunajifunza wakati Nabii Samuel alipofika katika nyumba ya Yese kumpaka mafuta mfalme mpya wa Israeli, Yese alimleta kwanza Eliabu mbele ya nabii Samuel, ambaye alikuwa mzaliwa wake wa kwanza. Yeye Eliabu alikuwa mtu mwenye nguvu na shujaa, hivyo alijiaminisha angekuwa mfalme mpya wa Israeli. Hata hivyo Mungu akasema, hapana, si yeye. Kwa hakika Eliabu alihisi kupuuzwa. Mfumo wote wa wakati huo ambao uliweka kipaumbele kwa mzaliwa kwa kwanza kurithishwa mambo yote ulionekana kana kwamba umepuuzwa. Hakuteuliwa kuwa mfalme. Badala yake kijana mdogo kabisa katika familia yao – ambaye hata hakufikiriwa, ndiye aliyetiwa mafuta kuwa mfalme.

Hakuna hata mtu mmoja asiyependa kuonekana kama siyo makini, hana uwezo

2 WAKORINTHO 5:17

HATA IMEKUWA, MTU AKIWA NDANI YA KRISTO AMEKUWA KIUMBE KIPYA; YA KALE YAMEPITA TAZAMA! YAMEKUWA MAPYA.

na hahitajiki katika jamii inayomzunguka. Hata kama hatupendi kuonekana hivyo, bado maoni ya wengine yana uzito sana. Neno la kukataliwa, hata kama ni dogo kiasi gani na hata kama halikutarajiwa lituumize, linaweza kudumu na kuumiza mioyo yetu. Mbegu ndogo sana ya kukataliwa yaweza kuota mizizi na kuleta maangamizi kwa wakati ujayo. Ghafla tunasahau kuwa Mungu alituumba kwa namna ya kipekee kwa kusudi lake na mpango wake kamilifu. Tunasahau kwamba Mungu hatutaki tujilinganishe na wengine au kukimbia mbio ya mtu mwingine. Tunasahau uumbaji wetu wa kimuujiza na kazi ya Yesu Kristo ya kutufanya kuwa kiumbe kipya (2 Wakorintho 5:17). Ghafla tunajikuta tukiteswa na jitu hili linaloitwa "kukataliwa."

Kuuona ushindi wa Yesu dhidi ya kukataliwa kunakuja kwa namna unavyojiona wewe jinsi Baba Mungu wa mbinguni anavyokuona – kama mtoto wake mpendwa akupendaye. Kama Paulo Mtume anavyoandika katika Warumi 8:17 ***"na kama tu watoto, basi, tu warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo; naam, tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye."*** Mungu hakukubali wewe kwa sababu ya jambo lolote ulilolifanya, hasha, lakini ni kwa sababu anakupenda (1 Yohana 4:19). Zaidi ya yote, Mungu alikupenda sana kiasi cha kutaka kukuleta karibu katika ushirika naye kupitia kifo cha mwanaye pekee, Yesu Kristo, pale msalabani.

Kumbuka, pamoja na ukuu wote wa Mungu, bado yeye anakukumbuka na kukujali sana (Zaburi 8). Amekutafuta na kukufuata (Luka 15:3-7).

Kabla hujatungwa mimba, Mungu anasema "nilikuchagua kuwa wangu." Ukweli huu ukupe ujasiri ndani ya moyo wako. Thamani yako haitokani na kile ulichoweza kufanya lakini ni imara katika ukweli kwamba Yesu alitolewa kwa ajili yetu. Umekubaliwa na kukumbatiwa na baba yako wa mbinguni. Upendo wa Mungu kwako ni wa bure kabisa. Unaishi kwa kukubaliwa naye siyo kwa kukubaliwa na wanadamu wengine. Unapotafakari haya, lile jitu la kukataliwa maishani mwako litaanguka na kutoweka kabisa.

ISAYA 49:15

JE! MWANAMKE AWEZA KUMSAHAU MTOTO WAKE ANYONYAYE, HATA ASIMHURUMIE MWANA WA TUMBO LAKE? NAAM, HAWA WAWEZA KUSAHAU, LAKINI MIMI SITAKUSAHAU WEWE

ANDIKO LA KUSIMAMIA

Warumi 8:15-16
Wagalatia 4:6-7

MAOMBI

[***Weka mikono yako kwenye kifua chako***]

[***Ni vizuri ukaomba maombi haya kwa sauti***]

BWANA Yesu Kristo, naamuru roho ya kukataliwa kutoweka. Watu wanaponikataa na kunitenga, marafiki wamenikataa na kunitenga, wazazi wangu au familia yangu imenitenga na kunitakaa. Roho hizi naziamuru kuondoka ndani yangu sasa kwa Jina la Yesu Kristo.

Naamuru roho ya kukataliwa na roho ya kujikataa mimi mwenyewe iondoke ndani yangu na kuniacha sasa na isirudi tena kwa Jina la Yesu Kristo.

Napokea kukubaliwa kutoka kwa BWANA Yesu Kristo. Wewe ni Baba yangu na natambua unanipenda. Naamuru kila pepo, majini, roho za mizimu, matambiko, uchawi na ushirikina zinazonishambulia kutoka sasa ndani yangu kwa Jina la Yesu Kristo. Naamuru roho zote chafu zinazoshambulia mwili wangu kuondoka ndani yangu na zisirudi tena kwa Jina la Yesu Kristo.

Navunja nguvu zote za magonjwa, udhaifu na mapungufu yoyote katika mwili wangu kwa Jina la Yesu Kristo na natumia damu ya Yesu Kristo kusafisha kila ambalo Mungu hajakusudia katika maisha yangu liondoke mara moja.

Naamuru yote yasiyo ya Mungu yaondoke sasa kwa Jina la Yesu. Kila aina ya udhaifu uondoke sasa kwa Jina la Yesu. Asante sana BWANA Yesu.

Navunja nguvu zozote za mapepo, majini na nguvu zote za giza zinazoniletea matatizo katika maisha yangu na kuziamuru ziondoke mara moja katika Jina la Yesu Kristo.

Namsamehe kila mmoja aliyenikosea na nakuomba Mungu uwabariki na kuwaokoa.

Naamuru kila roho inayonitesa iondoke ndani yangu. Kila roho chafu, mapepo na majini yaliyoamuriwa kuja kwangu na kunifanya nisiweze kusamehe, naiamuru iondoke na kuniachia sasa kwa Jina la Yesu Kristo na kamwe isirudi tena.

Naamuru roho yoyote isiyokuwa roho ya Mungu iondoke ndani yangu sasa kwa Jina la Yesu Kristo. Chuki, uchungu, hasira viondoke sasa. Naamrisha kuondoka ndani yangu kila roho ya upweke, roho zote za huzuni, kukata tamaa, utegemezi, aibu, kushindwa, kukata tamaa, kifo na kujiua, moyo mzito, huzuni, hasira, kuniachia sasa kwa Jina la Yesu Kristo.

Naamrisha kuondoka ndani yangu kwa Jina la Yesu kila roho iliyonisababisha nikauke katika mambo ya Mungu, kila roho iliyonitawala wakati ninapaswa niitawale na kuimiliki nchi.

Naamrisha kila roho inayoniadhibu iondoke sasa kwa Jina la Yesu na navunja nguvu zao kwa Jina la Yesu Kristo. Naamrisha kila roho ya ukichaa, kuchanganyikiwa, usahaulifu, kukamatwa mateka akili, kudhibiti akili, hisia mseto, mawazo mawili, dhiki, kudhoofu kwa akili, migogoro ya akili, wazimu, hofu ya watu, hofu ya wadudu, pepo wote wa akili, hofu ya aina yeyote ile, wasiwasi na woga, kuondoka ndani yangu na kuniacha huru kabisa kwa Jina la Yesu Kristo.

“Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi.” (2 Timotheo 1:7)

[***Pumua kwa ndani kisha kohoa nje kwa sababu mapepo yanatoka nje kwa njia ya pumzi, kupitia kinywa kwa njia ya kukohoa, n.k.***]

Muombe Mungu kukubatiza kwa Roho Mtakatifu kwa njia ya Jina la Yesu Kristo.

[***Ni muhimu sana ukashikilia muujiza wako wa uponyaji na kufunguliwa. Ebu chunguza nyumbani kwako, ofisini, bustanini, kwenye usafiri wako na kila mahali panapokuhusu kama kuna kitu chochote kinachotumika kama miungu ya kuabudiwa. Acha mara moja kusikiliza mafundisho ya uongo na kujishughulisha na mambo yatakayo kupotosha katika imani yako ndani ya Yesu Kristo na ufunge kabisa milango inayotumiwa na mapepo, majini, nguvu za kichawi, mizimu, ushirikina na nguvu zote za giza kukuvamia tena. Ebu soma habari ya “Kurejea kwa roho chafu katika Mathayo 12:44***]

SIKU YA NNE

ACHANA NA KUBWETEKA NA CHUKUA HATUA

Inaweza ikaonekana kama si jambo la kawaida kufikiria kubweteka au kutokuchukua hatua kama kitu kinachoweza kutudhihaki na kuumiza maisha yetu na hata kutufanya kutofikia malengo yetu. Wote tunapenda kuweka mazingira salama kwa ajili ya familia zetu. Baada ya shughuli nyingi za siku nzima na uchovu, tungependa kumaliza siku yetu kwa kuangalia kipindi kizuri cha kuchekesha kwenye luninga. Tunapenda kila jambo katika maisha yetu liwe katika mpangilio mzuri, na lisiwe katika machafuko. Yote haya si mabaya hata chembe. Ubaya ni pale shauku ya ulinzi na usalama wa maisha yetu ndio unakuwa kipaumbele cha kila jambo tunalolifanya.

MITHALI 1:32 (NENO)

KWA KUWA UKAIDI WA WAJINGA UTAWAUA, NAKO KURIDHIKA KWA WAJINGA KUTAWAANGAMIZA

Katika simulizi ya Daudi na Goliati, tunaona namna tamaa hii ilivyoligubika taifa la Israeli. Kila siku Waisraeli walikwenda mstari wa mbele wa vita. Walikuwa na Mungu upande wao. Hata hivyo katika siku arobaini walishindwa kusonga mbele na kupigana na Wafilisti kwa mtego wa kujifariji. Goliati alikuja kuwadhihaki Waisraeli kila asubuhi na Waisraeli walikuwa wakisema “Siyo leo. Ni hatari sana. Ngoja tukae katika hema ambapo ndipo kuna usalama.”

Picha tunayokosea kuipata katika simulizi hii ni kwamba Daudi alifika mahali

hapo na akafanya jambo katika siku moja ambalo jeshi zima la Waisraeli walishindwa kulifanya kwa kipindi cha zaidi ya mwezi mmoja. Kila siku walikuwa wakitetemeka. Kila siku tamaa ya usalama wao iliwarejesha nyuma na kushindwa kuchukua hatua. Kila siku lile jitu Goliati lilizidi kuja na kuwadhihaki. Ndipo Daudi akatokea na kusema, “huu ni ujinga. Hii lazima iishe siku ya leo.”

Mungu anapenda nawe pia uone zaidi ya hali yako ya kubweteka kwa usalama unaouhisi na utambue kuwa kuna jambo ambalo ni la umilele ambalo unapaswa kupambana nalo. Mungu anakuita kwa kusudi kubwa zaidi kuliko hali ya usalama wa kipindi kifupi unaouishi. Anataka kukupa ushawishi halisi. Anataka utembee katika njia za haki kwa ajili ya jina lake. Anataka utembee kwa utii kwa mapenzi yake. Mungu anakualika leo kujitayarisha, ujiunge katika mwito wake wa vita na kupambana na adui. Kumbuka, Mungu anachukia kubweteka na kutokuchukua hatua (Ufunuo 3:16)

UFUNUO 3:16 (NENO)

HIVYO KWA KUWA U VUGUVUGU, SI BARIDI WALA MOTO, NITAKUTAPIKA UTOKE KINYWANI MWANGU

Kupata ushindi dhidi ya jitu linaloitwa “kubweteka” kuna maanisha kujiunga na wito huu. Ina maanisha kukataa kusubiri mpaka mazingira muafaka yatakaporuhusu kabla ya kuchukua hatua. Ina maanisha kuwa tayari kwenda katika uelekeo ambao unaonekana sio uliozoeleka. Ina maanisha kuelewa kwanza kilicho muhimu kuliko yote ni kutembea katika nguvu ya Mungu kuliko kutegemea nguvu zako mwenyewe. Mara unapoelewa siri hii, basi uko tayari kwa vita. Uko tayari kupelekwa kwenye hatua ambayo utashuhudia wokovu wa Mungu.

Kumbuka imani inashamiri katika mazingira ya dhiki na uweza wa Mungu katika udhaifu wetu (2 Wakorintho 12:9). Msalaba ulileta maumivu makubwa kwa Yesu kwa namna ambayo wakati huo huo ulituletea wokovu na uhuru. Mara nyingi ni rahisi kukaa tu na kuamua kufuata mfano wa maisha ya mtu mwingine – kumwacha mtu mwingine “aliyeitwa” kwenda na kupambana na hatari hiyo. Lakini ukweli ni kwamba Mungu hajaita kila mmoja wetu kukwepa hatari ya ulimwengu unaopotea. Badala yake Mungu ametuita kwenda katika ulimwengu na upanga wa Roho Mtakatifu katika mikono yetu. Anatutaka tuseme

2 WAKORINTHO 12:9

...NEEMA YANGU YAKUTOSHA; MAANA UWEZA WANGU HUTIMILIKA KATIKA UDHAIFU. BASI NITAJISIFIA UDHAIFU WANGU KWA FURAHA NYINGI, ILI UWEZA WA KRISTO UKAE JUU YANGU

"imetupasa kuzifanya kazi zake yeye aliyenipeleka maadamu ni mchana, usiku waja asipoweza mtu kufanya kazi." (Yohana 9:4).

Maisha yako hapa duniani ni mafupi, lakini Mungu ni Mkuu. Hivyo, zingatia sana mambo muhimu yahusuyo uzima wa milele wakati ungali mzima. Unaishi ulimwenguni ambapo mabilioni ya watu hawamfahamu Yesu Kristo. Kama mfuasi wa Yesu unalo tumaini.

Tunapaswa kutambua kuwa moja ya hatari kubwa sana kwa maisha ya mkristo ni "kubweteka" na hivyo kutokuchukua hatua. Ina maanisha kuwa unajiona umetosheka kwa juhudi na matokeo uliyoyapata katika kumtafuta na kumtumikia Yesu Kristo, hivyo hufanyi tena juhudi za kumtafuta Mungu zaidi na hivyo kuendelea kuishi kwa ushindi na mafanikio yako ya zamani.

Baadhi ya madhara kwa mkristo au hata Mtumishi wa Mungu kubweteka ni pamoja na yafuatayo:

Kubweteka ni hatari sana kwa Mkristo kwa sababu inamaanisha haukui tena katika mambo ya Mungu.

Biblia iko wazi kabisa kuhusu madhara ya Wakristo kutokupiga hatua mbele katika mambo ya Mungu. Tuna chaguzi mbili tu, aidha tunakua katika mambo ya Mungu au tunarudi nyuma. Baada ya kuainisha tabia ambazo kila Mkristo anapaswa kuwa nazo, Petro anaeleza ***"Maana mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala si watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo."*** (2 Petro 1:8). Kwa maneno mengine, kama wewe ni mkristo uliyebweteka au mvivu kwa kukua kwako kwa mambo ya Mungu, uko katika hatari kubwa.

Kubweteka ni hatari sana kwa sababu kunasababisha tuishi kwa kujifariji kwa ushindi wetu tulioupata au mafanikio tuliyoyapata zama zilizopita.

Wakristo wanapaswa kumtafuta Kristo, na tukifanya hivyo anatupa ushindi. Hatari ni pale tunapotegemea ushindi au mafanikio tuliyoyapata katika zama zilizopita. Kubweteka kunatupa jaribu la kukumbuka mafanikio yetu ya zamani wakati tunapaswa kuangalia vita iliyo mbele yetu ambayo Mungu anatutaka tuishinde kwa ajili ya utukufu wake.

Mara nyingi tunaona nguvu za Mungu katika maisha yetu na kudhani kuwa kwa sababu alitutendea namna hiyo, basi atatenda mara tena kwa njia hiyo hiyo. Tunaanza kubweteka katika imani yetu tunapofikiria ushindi aliotupa Mungu zamani na kushindwa kumtafuta Mungu kwa changamoto za sasa na za baadaye.

Kubweteka Kunazuia Maisha ya Maombi ya Mkristo, Kitu Ambacho ni Hatari Sana.

Haijalishi wewe ni nani, haijalishi Mungu amefanya nini kupitia wewe, haijalishi ni huduma yenye nguvu kiasi gani uliyoiongoza, wewe una nguvu tu za Mungu na unaweza kutumika na Mungu kwa kadri unavyojitoa katika maisha ya maombi. Kwa mfano, Mfalme Daudi alifanya mambo mengi ya kushangaza kabla ya kutenda dhambi na Bathsheba. Alikuwa mpakwa mafuta wa BWANA, akashinda vita vingi na alikuwa mfalme mkuu wa Israel, lakini hayo yote hayakumzuia kuzini.

Kama umekuwa ukihudhuria kanisani kwa miaka kadhaa, kwa vyovyote vile utakuwa umesikia mmoja wa viongozi wa kikristo mwenye jina na sifa kubwa ameanguka katika dhambi au ameacha kabisa imani. Kitu kinachochanganya ni kuwa ingawa viongozi hawa wa dini walipotoka, walikuwa wakitumiwa sana na Mungu kumletea utukufu. Je, kuanguka kwa Mchungaji kunaondoa mambo yote mazuri ya Mungu ambayo Mchungaji huyo aliyafanya huko nyuma? Hapana. Hata hivyo, inadhihirisha kuwa mafanikio ya zamani katika Mungu hayawezi kudumu kama tusipoendelea kumtafuta Mungu kwa ajili ya changamoto za sasa na zilizo mbele yetu. Ukweli ni kwamba, kabla ya Mchungaji huyu kuanguka, alianza kuwa na maisha ya kutokujihusisha na maombi kwa sababu ya kubweteka katika Kristo.

1 NYAKATI 16:11

MTAKENI BWANA NA NGUVU ZAKE; UTAFUTENI USO WAKE SIKU ZOTE

Lazima tumtafute Mungu daima, tukiombea mambo yote kwa wakati wote – hata pale maombi yetu hapo awali yalijibiwa au tulishuhudia Mungu akitutumia kwa kiwango kikubwa sana. Ukweli ni kwamba, pale Mungu anapotutumia kwa viwango vikubwa sana ndipo tunapopaswa pia kuzidisha kumtafuta Mungu zaidi na kuongeza maombi katika maisha yetu.

Ili kuepuka kupiga mwendo usiokuwa na tija, tunapaswa kutambua kuwa tunaweza kuwa vyombo vizuri kwa Mungu pale tunapomtafuta kila wakati na

kuyajua mapenzi yake kwetu. Tukiendelea kuishi kwa kujifariji kwa kukumbuka namna Mungu alivyotutumia zamani, tutakuwa tumejiweka katika hatari kubwa ya kuanguka. Lazima tumtafute kila iitwapo leo kama tunatarajia kuvipiga vita na kuvimaliza vizuri kwa ushindi mkubwa.

Kubweteka ni janga kubwa kwa kila mkristo. Tumwombe Roho Mtakatifu atulinde dhidi ya roho hiyo kwa kuishi maisha ya kujifariji kwa ushindi wetu wa zamani huku tukishindwa kumtafuta Mungu kwa changamoto za sasa na zijazo mbele yetu. Dawa pekee dhidi ya ugonjwa wa kubweteka ni kumtafuta Yesu Kristo kwa bidii. Neno la Mungu linasema ***"Mtafuteni BWANA, maandamu anapatikana, mwiteni maadamu yu karibu"*** (Isaya 55:6)

Unaufahamu ukweli. Unao uzima. Unaye Yesu. Hayo ndiyo muhimu sana: mwache Yesu ajulikane kwa ulimwengu. Hivyo basi ondoka, ingia vitani kwa jina la Yesu Kristo.

ANDIKO LA KUSIMAMIA

Marko 8:34-35

MAOMBI

Utenzi huu ***MAOMBI DHIDI YA KUBETWEKA KWA MKRISTO*** ulitungwa na Sir. Francis Drake (1540 – 28 January 1596) ambaye alikuwa Nahodha Mwingereza, Afisa wa Jeshi la Maji wakati wa Enzi za Malkia Elizabeth I (1558–1603) na aliyezunguka dunia katika safari moja kati ya mwaka 1577 hadi 1580. Utenzi huu waweza pia kuufanya kama maombi yako. (Tafsiri hii ni ya kwetu)

TUPE CHANGAMOTO

Tupe changamoto, BWANA
Pale tunapokuwa tumebetweka na kujifariji,
Pale ndoto zetu zinapojibiwa
Kwa sababu maono yetu yalikuwa madogo mno,
Tulipofika salama
Kwa sababu tulisafiri karibu sana na ufukwe.

Tupe changamoto, BWANA
Pale, tunapokuwa na umiliki wa vitu vingi,
Tumepoteza shauku yetu
Ya maji ya uzima;
Tulipopenda maisha ya dunia hii,
Tukasahau kuutafuta ufalme wa milele,
Na katika juhudi za kuujenga ufalme wetu wa dunia,
Tumeruhusu maono yetu
Ya Mbingu mpya kufifia.

Tupe changamoto, BWANA, kuwa na ujasiri zaidi,
Kwenda katika vilindi vya bahari iliyochafuka,
Ambapo mawimbi yatatuonyesha Uumbaji wako wa ajabu;
Ambapo kutoiona ardhi,
Kutatufanya tuone na kushangaa nyota ulizoumba,

Tunakuomba uturejeshee,
Maono ya matumaini yetu,
Na kuturejeshea hatima yetu ya baadaye,
Kwa nguvu, mamlaka, ushujaa, tumaini na upendo.

Tunaomba haya katika Jina la Nahodha wetu,
Ambaye ni Yesu Kristo (Amina).

SIKU YA TANO

LAZIMA TUITIISHE HASIRA

Katika simulizi ya Daudi na Goliati, hatuoni hasira kutoka kwa Daudi. Tunachoona ni watu wengi walio na hasira waliomzunguka. Mmoja kati ya watu hao, kama tulivyoona awali, ni kaka yake mkubwa, aliyewaka kwa hasira dhidi ya Daudi (1Samuel 17:28). Eliabu angepaswa kuwa wa msaada kwa Daudi alipofika mstari wa mbele wa vita. Lakini hasira ndani ya moyo wake ilikuwa ikijijenga kwa muda mrefu, ikisubiri fursa ya kujitokeza. Na kweli hasira hiyo ikajitokeza.

WAEFESO 4:26

MWE NA HASIRA, ILA MSITENDE DHAMBI; JUA LISICHWE NA UCHUNGU WENU BADO HAUJAWATOKA

Si kila hasira ni mbaya. Biblia inaonyesha kuna wakati wa kuwa na hasira na wakati muafaka wa kuonyesha hasira yako (Yakobo 1:19). Kuna wakati hata Yesu alihisi hasira (Marko 3:5). Hata hivyo, hasira inakuwa jitu pale inapofanya kazi ndani yako na kujitokeza nje kwa kusudi la uovu, kama ilivyotokea kwa Eliabu.

ZABURI 37:8

UKOMESHE HASIRA, UACHE GHADHABU, USIKASIRIKE, MWISHO WAKE NI KUTENDA MABAYA

Moja ya namna ya kujielewa kuhusu hili ni pale unapohisi hasira kwa jambo ambalo halikutokea. Labda unahisi rafiki yako alifanya jambo dhidi yako, wakati ukweli ni kwamba hajafanya jambo hilo. Ulihisi hasira kwa jambo ambalo halikutendeka dhidi yako. Wakati mwingine waweza kuwa na sababu sahihi ya

kuhisi hasira lakini ukaionyesha hasira hiyo kwa njia ambayo si sahihi. Kama Eliabu, hasira yako iliyojificha unaionyesha na kuwakwaza wengine. Wakati mwingine una sababu sahihi ya kuonyesha hasira yako, lakini ukaendelea kuiweka moyoni mwako. Kuendelea kuiweka hasira yako moyoni ina matokeo hasi kwa afya yako na kwa ukweli ni moja ya vitu vibaya sana unavyoweza kufanya.

MITHALI 26:20

MOTO HUFA KWA KUKOSA KUNI; NA BILA MCHOCHEZI FITINA HUKOMA

Kwa hiyo, unawezaje kuishinda hasira? Unawezaje kuwa mshindi kupitia ushindi ambao Yesu amekwisha kukushindia? Inaanza kwa kuelewa kwamba mabadiliko ya kudumu hayaji papo kwa papo. Mara nyingi, Mungu hubadili maisha yako kidogo kidogo. Funguo wa kweli katika mabadiliko ya kiroho ya maisha yako ni kila siku kuishi maisha ya imani na kuendelea kuuishia wokovu, ile kazi ambayo Yesu anaendelea kuifanya maishani mwako. Soma Neno la Mungu na badilisha hasira yako ili maisha yako yaendane na ukweli unaousoma katika Neno la Mungu. Badilisha maongezi uliyo nayo ya hasira katika akili yako kwa kuwaombea wote waliokukwaza. Jielekeze katika mpango wa Mungu na mwite Yesu kutawala kabisa moyo wako.

Inasaidia unapojikumbusha kwamba wewe si mkamilifu. Mungu alikwisha kukusamehe kwa hiyo unaweza kuwasamehe wengine (Luka 11:4). Mungu amefanya amani nawe kupitia Yesu Kristo msalabani, kwa hiyo unapokuwa na hasira, kimbilia msalabani. Elewa kuwa Mungu ndiye anayekulipia kisasi (Warumi 12:19) na amekuweka huru ili ufanye amani na wengine. Tambua kwamba alichokufanyia Yesu ni kikubwa sana kuliko anachoweza kufanya mtu yeyote dhidi yako. Kwa nguvu ya Yesu, inawezekana kusamehe wale ulio na hasira dhidi yao na hivyo kuyaondoa maumivu kutoka katika moyo wako ambayo yamegeuka kuwa sumu kali ya maisha yako.

Ni muhimu pia kuelewa kuwa wewe ni mwana wa Mungu (Yohana 1:12). Jikumbushe kila siku kuhusiana na ukweli huu. Unaweza kuwa umekataliwa na wengine na ukajiona kuwa si wa muhimu, lakini kwa macho ya Mungu anakupenda, uko salama, mzima na wa muhimu sana. Acha sauti ya Yesu iongee zaidi ya sauti zingine zote zinazojaribu kuchukua nafasi ya kwanza katika maisha yako.

Mwishowe, kuishinda hasira ni kuacha wewe kuwa mdhibiti wa hali hiyo. Fanya kama alichokifanya Daudi na jikite zaidi kwa Mungu kuliko watu waliokufanyia

mabaya. Unapofanya hivyo utawekwa huru na utasonga mbele kwa nguvu ya Mungu kufanya kile ambacho Mungu amekuitia.

ANDIKO LA KUSIMAMIA

Yakobo 1:19-20

MAOMBI

Eeh Mungu wangu, nisamehe dhambi zangu zote nilizozitenda, ikiwa pamoja na eneo la hasira, katika Jina la Yesu. Mungu wangu, nihurumie na usafishe dhambi zangu zote kwa Jina la Yesu Kristo. Baba, iwapo roho ya hasira ni ya asili ya kuzaliwa nayo, iondoe kutoka kwangu, kwa Jina la Yesu Kristo. Chochote kile ambacho roho ya hasira imeharibu katika maisha yangu (***.....endapo unavikumbuka basi vitaje vyote***), eeh Mungu wangu, anza kuvikarabati kwa huruma zako na katika Jina la Yesu Kristo.

Baba, naomba amani yako itawale akili na mawazo yangu, katika Jina la Yesu. Aina yoyote ya nguvu za uharibifu inayovamia ubongo na akili yangu, viharibiwe katika Jina la Yesu Kristo.

Baba yangu, niko hapa nikiwa tayari kwa ajili ya matengenezo ya tabia yangu na mwenendo wangu. Nitengeneze upya tena kwa Jina la Yesu Kristo. Naharibu kila mshale wa hasira katika Jina la Yesu Kristo na kuharibu roho zote za hasira kwa nguvu na uweza wa damu ya Yesu. Hasira ya kuchochewa na malipizi, toka ndani yangu katika Jina la Yesu Kristo.

Kila nguvu inayotaka kuharibu baraka zangu ife katika Jina la Yesu Kristo. Tabia yangu imeharibiwa na nguvu za giza kupitia roho ya hasira. Naharibu mipango yote ya ibilisi katika maisha yangu kwa Jina la Yesu Kristo.

BWANA Yesu, niokoe kutoka katika mateso ya hasira ya uchochezi na malipizi, katika Jina la Yesu Kristo. Najiondoa kutoka katika tabia ya hasira katika Jina la Yesu. Umba ndani yangu eeh BWANA Yesu, moyo safi.

Baba yangu, naomba uondoe sasa roho ya hasira na usiiache initawale, katika Jina la Yesu Kristo. Eeh BWANA wangu, wale ambao wamekwazika kwa sababu ya hasira yangu, nisamehe, katika Jina la Yesu Kristo. Roho Mtakatifu, kamata

moyo na roho yangu, katika Jina la Yesu Kristo. Kila pepo wa Delila aliyeko ndani yangu anayesababisha nipandishe hasira dhidi ya mume wangu (au mke wangu) (au ndugu zangu), eeh BWANA, naomba uiondoe kwa nguvu na uweza wa damu ya Yesu.

Kila mtu anayetumia udhaifu wangu huu kwenda kinyume changu, Eeh Baba, urekebishe kwa moto wa Roho Mtakatifu na kwa nguvu na uweza wa damu ya Yesu Kristo. Eeh BWANA, achilie hasira yako takatifu ipoze roho yangu ya hasira, katika Jina la Yesu Kristo. Kila roho ya kiburi ndani yangu, naiondoa katika Jina la Yesu Kristo. Nailaani kila roho ya hasira na chuki katika maisha yangu na kuiondoa katika Jina la Yesu Kristo. Naisihi damu ya Yesu itawale kila tabia yangu mbaya.

BWANA Yesu, safisha hasira yangu kwa damu ya Yesu. Kila kitu ambacho hakikukusudiwa kuwa katika maisha yangu na mwili wangu, ondoka sasa kwa Jina la Yesu Kristo. Ondoka katika kichwa changu, moyo wangu, roho yangu, uso wangu, kwa Jina la Yesu Kristo. Naamuru kila pepo linaloniathiri kupitia roho hii ya hasira, ondoka sasa katika maisha yangu kwa Jina la Yesu Kristo. Kila hasira ya kurithi kutoka kwa wazazi na ukoo wangu, naivunja sasa kwa damu ya Yesu Kristo.

Roho ya hasira inayonyemelea ndoa yangu, nakuchoma kwa moto wa Roho Mtakatifu na kwa Jina la Yesu Kristo. Wewe hasira, najiondoa kwako sasa katika Jina la Yesu. Ndoa yangu haitavunjika au kuharibika kwa sababu ya hasira zangu, kwa Jina la Yesu Kristo.

Kila mpango wa adui wa kunifanya nifukuzwe kazi yangu kwa sababu ya pepo chafu ya hasira, wewe ni muongo. Natubu kila tabia yangu mbaya leo kwa Jina la Yesu Kristo. Nabadilisha hasira yangu ya uovu kuwa hasira takatifu ya BWANA wetu Yesu Kristo. Kinywa changu hakitanifanya nitamke maneno yatakayoniletea mabaya. Kila nguvu ya giza niliyopandikiziwa ili kuchanganya akili na mawazo yangu kila mara ninapozungumza, naiteka nyara sasa kwa Jina la Yesu Kristo.

Sitatumia kinywa changu kutawanya baraka za Mungu katika maisha yangu. Baba yangu, nitangaze kama mtu mwema kwa watu wengine, kwa Jina la Yesu Kristo. Kila tunda la hasira linalonisababishia kunuka mbele ya watu wengine, Baba Mungu na BWANA wangu, naiteka nyara hiyo roho kwa Jina la Yesu Kristo. Kila tendo la uovu lililofanywa kwa makusudi na watu ili waweze kuniteka, naliharibu

kwa damu ya Yesu Kristo. Kila roho ya kukosa uvumilivu, naifisha katika maisha yangu kwa Jina la Yesu Kristo. Roho ya kiburi katika maisha yangu, naipiga moto kwa Jina la Yesu. Nakataa kutawanya nyumba na wote waliomo katika nyumba yangu kwa ajili ya hasira zangu na ugomvi ninaosababisha kila wakati katika Jina la Yesu.

Sasa natangaza uhuru dhidi ya roho zote za hasira na kiburi kwa Jina la Yesu Kristo. Nimekuwa huru na nimekombolewa kutoka katika roho zote chafu za ibilisi na mawakala wote waliokuwa wameniteka na kunitumikisha kupitia roho za hasira.

Katika Jina la Yesu nimeomba na kuamini, Amina.

SIKU YA SITA

URAIBU LAZIMA UTOWEKE

Wakati Daudi alipoamua kupigana na Goliati, Mfalme Sauli alimwambia "hana uwezo" (1Samuel 17:33). Akaendelea kwa kuelezea kwamba Daudi asingeweza kumpiga kwa sababu Goliati "ni mtu wa vita tangu ujana wake" na kwamba Daudi ni kijana tu. Daudi alipokataa kushawishiwa na visingizio hivyo, Sauli alijaribu kumlinda kwa silaha zake. Kwa kumvika mavazi hayo ya kivita (yaani chapeo kichwani na dirii) alitaka Daudi aonekane mwenye nguvu na aliyelindwa zaidi tofauti na hali yake ya uhalisia.

Mara nyingi tunafanya haya pia katika maisha yetu. Tunajiona hatuna nguvu katika dunia hii iliyoharibika na iliyo na mashambulizi mengi, hivyo tunajivika silaha za uwongo na kujificha ndani ya uraibu (***addiction***) au kwa Kiswahili cha vijana wa mtaani, ***uteja***. Ukweli unaouma ni kwamba kizazi chetu kimejikita kwenye uraibu. Twaweza kufikiria kwamba hatujaathirika na tabia hii, lakini ukweli ni kwamba kila mmoja wetu ana jambo ambalo anafikiri hawezi kuishi bila kuwa nalo au kulifanya. Yaweza kuwa ni pombe, mahusiano, kufanya manunuzi, mafanikio, kujipamba, sigara, madawa ya kulevya, na hata mitandao ya kijamii. Tumewekwa utumwa katika mambo haya na tunashindwa kuachana na tabia ya kuyafanya mara tunapohisi haja ya kupata faraja.

Tabia hii ya uraibu inaweza kukuondolea jambo jema ambalo Mungu amelipanga kwa ajili yako. Inaweza kukuongoza katika njia ambayo ile ahadi yako haiwezi kutimilizwa. Hatima yake, itakuathiri vibaya, itakudhihaki na kufifisha umaarufu na utukufu wa Mungu katika maisha yako. Kwa hiyo, unawezaje kupata ushindi

wa Yesu dhidi ya jabali hili?

MAOMBOLEZO 3:40

NA TUCHUNGUZE NJIA ZETU NA KUZIJARIBU, NA KUMRUDIA BWANA TENA

La msingi ni kuchunguza chanzo cha athari hiyo na si matokeo yake. Jiulize, chanzo cha machafuko haya katika maisha yangu ni nini? Kwa nini najihisi siwezi? Kwa nini naogopa kufahamika? Machungu yanatoka wapi? Usipokuwa tayari kujihoji na kugundua chanzo cha matatizo yako, jabali hili la uraibu haliwezi kuanguka kamwe.

Wengi wetu wanafuata mkondo ambao tunahisi hatuna uwezo wa kuushambulia, hali inayotufanya kujiona wanyonge. Unyonge huu unatulazimisha kujificha na kushindwa kupambana na hali halisi hivyo kutupelekea kwenye uraibu. Kwa bahati nzuri kuna suluhisho. Badala ya kukimbilia kwenye uraibu tunapohisi umuhimu wa kujificha dhidi ya tatizo linalotukabili, kimbilia kwa Yesu Kristo. Tambua kwamba unyonge wowote unaojihisi, Yesu Kristo hatakuacha. Anakupokea katika upendo wake na kukupa uhai wake. Anabadili unyonge wako kwa nguvu zake. Uwapo mnyonge, Yesu Kristo anaweza.

TITO 2:11-12

KWA MAANA NEEMA YA MUNGU IWAOKOAYO WANADAMU WOTE IMEFUNULIWA; NAYO YATUFUNDISHA KUKATAA UBAYA NA TAMAA ZA KIDUNIA; TUPATE KUISHI KWA KIASI, NA HAKI, NA UTAUWA, KATIKA ULIMWENGU HUU WA SASA

Labda uongo mkubwa kabisa unapokutana na uraibu ni kufikiria kwamba unaweza kupambana kwa nguvu zako mwenyewe huku ukiwa umejificha. Wakati wote kumbuka uhuru hutokea unapokuwa katika nuru. Yesu Kristo ndiye nuru ya dunia na hufanya kazi ndani yako kwa nguvu zaidi unapoleta udhaifu na kuumizwa kwako katika nuru ya rehema yake. Uko huru ndani ya Yesu Kristo mara tu unapoweka tumaini kwake. Yumkini unahitaji kuwa na watu ambao watakusaidia kuyafunua yote unayoyapitia. Fanya lolote lile ambalo ni la lazima kuyafanya maisha yako yawe katika hali ya uwazi, uaminifu na

WARUMI 7:18-19

KWA MAANA NAJUA YA KUWA NDANI YANGU, YAANI, NDANI YA MWILI WANGU, HALIKAI NENO JEMA; KWA KUWA KUTAKA NATAKA, BALI KUTENDA LILIO JEMA SIPATI. KWA MAANA LILE JEMA NILIPENDALO, SILITENDI; BALI LILE BAYA NISILOLIPENDA NDILO NILITENDALO

uwajibikaji.

Mwisho wa yote, Daudi alikataa kuvikwa yale mavazi ya kivita ya Sauli. Badala yake alichagua kumtegemea Mungu pekee. Akatoka kwenda kupigana na Goliati akiwa tu na kombeo, fimbo na Mungu wake, na akamshinda. Huu ni mfano wa maisha tunayopaswa kuishi, tunapomtegemea Mungu pekee kutupa nguvu katika unyonge wetu, jabali la uraibu litaanguka kutoka katika maisha yetu.

ANDIKO LA KUSIMAMIA

1 Wakorintho 10:12-13

MAOMBI

Mungu Baba, ninacho fahamu ni kuwa kwako wewe kila jambo linawezekana. Kwa unyenyekevu nakusihi usikie maombi yangu katika wakati wangu huu wa mahitaji. Naomba unisamehe na uniponye kabisa katika Jina la Yesu ili niweze kuushinda huu uraibu ninao shindana nao. Nimechagua kusalimisha moyo, mwili na nafsi yangu kwako, kukutumikia na kukuheshimu, nikikataa kuwa mtumwa wa uraibu. Kwa msaada wako na kwa nguvu ya Roho Mtakatifu nitapigana na kuushinda uraibu kwa nguvu zako, na si kwa nguvu zangu na nitawekwa huru kwa Jina la Yesu Kristo.

BABA yangu wa Mbinguni, nisaidie niweze kuwa na nidhamu binafsi itakayonifanikisha kuishinda hii roho chafu ya pepo wa uraibu inayonikabili. Nitaendelea kuamini katika upendo wako usio na kikomo na neema yako haitatufanya tushindwe. Rehema zako ni mpya kila siku na zadumu milele.

Baba, nakuja kwako, maana sina mwingine wa kukimbilia.
Ninatubu
Nimekaribia kabisa kupoteza maisha yangu, mwili wangu, nafsi yangu kupitia uraibu
Lakini pamoja na kuutambua uraibu huu hakujaniwezesha kuushinda.

Unaujua uraibu ninaopitia
Na haujawahi kunilaumu kwa kujiingiza katika uraibu
Unajua ukweli

Nilichukulia uraibu kama jambo la msaada wakati napitia wakati mgumu
Niliangukia kwenye uraibu kwa sababu nilikuwa najaribu kukimbia maumivu ya maisha
Pia nilitaka kujaribu kitu kipya ambacho nilidhani kingenipa uzoefu mpya
Na nikajikuta nimetumbukia kwenye shimo la uraibu na nikashindwa kujikwamua

Lakini sasa natambua kuna njia njema zaidi ya kuyakimbia maumivu ya maisha
Na kuna njia njema zaidi ya kushindana na changamoto zote za maisha
Naweza kupokea wito wa kweli kutoka kwako

Kwa sababu hiyo, najitoa kwako ili niweze kupokea sawasawa na uliyoyakusudia kwangu
Naomba sasa, na kwa wakati huu, Baba yangu wa Mbinguni, kwamba uniite kwa sauti yako kuu.

Uniite na uniinue kutoka katika hali hii ya uraibu na kunisimamisha katika utumishi wako
Na unaponiinua
Pia wakumbuke wengine wanaotaabika na hali hii ya uraibu nao pia uwainue na kuwaondoa katika mateso haya

Pamoja tunaweza kuinuka, kama nguvu moja pamoja nawe, mmoja baada ya mwingine, pamoja nawe
Uniinue kwa sababu nastahili maisha bora
Uniinue kwa sababu niko tayari kuinuliwa
Uniinue kwa sababu dunia inanihitaji

Nainuka na naendelea kuinuka; sitaanguka
Nainuka kwa sababu unanihitaji
Mimi ni sauti yako, ni mikono yako,
Nafurahia katika utakatifu niliorithi kutoka kwako
Kwa sababu mimi ni hekalu lako takatifu

Unaniinua kwa sababu nimekuomba na kwa sababu unanipenda sana
Kwa neema na rehema zako, nakuomba unisamehe yote niliyokukosea na kusafisha dhambi zangu zote
Akili yangu na nguvu zangu zote ziambatane nawe
Kwa rehema zako, uwezo wa akili zangu

Uongezwe zaidi kwa ajili ya kukutumikia kwa ukamilifu

Nikisimama katika mapenzi yako, nina nguvu na uweza wa kushinda nguvu zote za giza na vitu vyote vinavyonipeleka katika uraibu
Pamoja tunatengeneza mfereji wa upendo

Upendo wako unafikia hata hitaji langu la kushindana na uraibu na kuponywa
Kwa kuponywa kwangu, nasaidia dunia inayosumbuka katika uraibu kuponywa pia
Furaha yaujaza moyo wangu. Shukrani yangu haina kipimo na ni ya milele

Asante Mungu Muumbaji mwema
Na itakuwa hivyo
Katika Jina la BWANA wetu Yesu Kristo
Amina

SIKU YA SABA

UPOFU LAZIMA UONDOKE

Kuna vitu vingi katika maisha yetu ya kila siku vinatutesa na kutupatia shida mbalimbali na hivyo kutufanya tuishi maisha ambayo hatukustahili kuyaishi kwa sababu tu ya upofu. Upofu huu unaweza kuwa wa aina nyingi, ikiwa ni pamoja na upofu wa akili, ambapo huchukui nafasi kuishughulisha akili yako kufikiria na kutenda mambo ambayo yanaweza kukunufaisha au kukufanikisha katika maisha yako, kizazi chako na nchi yako kwa ujumla. Kwa msemo wa siku hizi, unashindwa kutumia fursa zilizopo na hivyo kuendelea kuishi maisha ya taabu, huzuni na dhiki kubwa huku ukiilaumu Serikali, ndugu zako, kanisa lako au jamii inayokuzunguka. Huna muda wa kutafakari namna gani utoke katika hali uliyo nayo sasa ili ufikie mafanikio kama wengine. Wewe ni mtu wa kuridhika tu na hali uliyo nayo, huhitaji cha ziada, kupiga hatua nyingine ya maendeleo. Huu ni upofu wa akili au fikra.

Upofu mwingine ni ule wa moyo. Kuna wakati moyo unakusukuma kufanya jambo ambalo ni jema, la maendeleo na manufaa kwako na kwa jamii yako, lakini unaogopa kuthubutu kuchukua hatua. Hofu ya kuthubutu inakuzalishia upofu wa moyo na haki yako hatimaye inamilikiwa na adui yako.

Upofu mwingine ni ule wa roho, ambao huu ndio upofu mbaya zaidi. Neno la Mungu katika 2 Wakorintho 4:3- linasema ***"Lakini ikiwa injili yetu imesitirika, imesitirika kwa hao wanaopotea; ambao ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu. Kwa maana hatujihubiri wenyewe,***

WARUMI 1:20-22

KWA SABABU MAMBO YAKE YASIYOONEKANA TANGU KUUMBWA ULIMWENGU YANAONEKANA, NA KUFAHAMIKA KWA KAZI ZAKE; YAANI, UWEZA WAKE WA MILELE NA UUNGU WAKE; HATA WASIWE NA UDHURU; KWA SABABU, WALIPOMJUA MUNGU HAWAKUMTUKUZA KAMA NDIYE MUNGU WALA KUMSHUKURU; BALI WALIPOTEA KATIKA UZUSHI WAO, NA MIOYO YAO YENYE UJINGA IKATIWA GIZA. WAKIJINENA KUWA WENYE HEKIMA WALIPUMBAZIKA

bali Kristo Yesu ya kuwa ni Bwana; na sisi wenyewe kuwa tu watumishi wenu kwa ajili ya Yesu. Kwa kuwa Mungu, aliyesema, Nuru itang'aa toka gizani, ndiye aliyeng'aa mioyoni mwetu, atupe nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo." Macho yetu ya mwili yameumbwa kuona mambo ya mwilini tu, lakini kwa habari ya mambo ya rohoni, tunapaswa kumwomba Mungu atupe macho ya rohoni, ambayo ndio yanatufanya tuyaone mambo makuu ya Mungu aliyotufunulia katika ulimwengu wa roho.

Katika kisa cha Daudi na Goliati, hofu waliyokuwa nayo wana wa Israeli na Mfalme wao Sauli iliwapa upofu wa kutokujua kwamba Mungu wao ni mkuu sana na ana jeshi liwezalo kumshinda adui yoyote yule (Yoshua 5:13-15). Kwa hiyo, wakashindwa kuthubutu na kuchukua hatua ya kupambana na Goliati, na kila mara Goliati alipojitokeza wote walikimbia (1Samuel 17:24).

Hata hivyo, Daudi, kwa kutambua kuwa Mungu aliye upande wake ni mkuu sana kuliko Wafilisti na shujaa wao Goliati, akauliza "***...Je! Atafanyiwaje yeye atakayemwua Mfilisti huyo, na kuwaondolea Israeli aibu hii? Maana Mfilisti huyu asiyetahiriwa ni nani hata awatukane majeshi ya Mungu aliye hai?"*** (1Samuel 17:26).

Haijalishi changamoto unayokutana nayo au unayoipitia ni kubwa kiasi gani na haijalishi kwamba mazingira yote yanaonyesha kuwa hutaweza lolote katika kushinda changamoto hiyo, fahamu kuwa Mungu ni mkuu sana na iangalie changamoto hiyo kwa macho ya kiroho na kuamini kuwa ushindi ni lazima kwa mwana wa Mungu. Hivi ndivyo ilivyokuwa kwa Elisha na mtumishi wake walivyozingirwa na majeshi ya mfalme wa Shamu. Yule mtumishi alipoingiwa na hofu kuu, Elisha akamtia moyo na

WAFILIPI 4:13

NAYAWEZA MAMBO YOTE KATIKA YEYE ANITIAYE NGUVU

kumwambia ***"usiogope, maana walio pamoja nasi ni wengi kuliko wale walio pamoja nao"*** (2 Wafalme 6 :16). Ili kuthibitisha neno lake, Elisha akamuomba Mungu amwondolee upofu yule mtumishi kwa kumfumbua macho yake na yule mtumishi akaona ***"na tazama, kile kilima kilikuwa kimejaa farasi na magari ya moto yaliyomzunguka Elisha pande zote"*** (2 Wafalme 6:17).

Kama watoto wa Mungu tunapaswa tutambue kuwa Mungu akiwa upande wetu basi hakuna awezaye kuwa juu yetu (Warumi 8:31). Inapaswa tuishi maisha ya ushindi kila wakati. Tukiendelea kuishi katika maisha ya upofu wa akili (fikra) au moyo basi tusitarajie maisha yenye kupiga hatua ya kimaendeleo na kuishi maisha ya kushinda changamoto zinazotukabili kila siku. Lazima tukubali kubadilika ili kuweza kuona fursa ndani ya changamoto hizo.

Fursa zilizokuwepo katika changamoto ya kupigana na kumshinda Goliati ilikuwa ni pamoja na Mfalme (1) kumtajirisha mtu huyo kwa utajiri mwingi; (2) kumwozesha binti yake; na (3) kumsamehe kulipa kodi yeye na familia yake yote (1 Samuel 17:25).

Aidha, pamoja na changamoto kubwa za mji wa Hebroni kukaliwa na Waanaki, Kalebu, akiwa na miaka themanini na tano, alimwendea Yoshua na kumuomba ampe urithi wa mji huo sawasawa na neno la Musa alilomuahidi wakati huo Kalebu akiwa na miaka arobaini tu (Yoshua 14:6-14). Kalebu alitambua wazi moyoni mwake kuwa, pamoja na Waanaki kuwa majitu na wazoefu wa vita, ataweza kuwaondoa katika nchi hiyo kwa msaada wa Mungu aliye hai.

ANDIKO LA KUSIMAMIA

2 Wafalme 6:8-20
Warumi 8:31
Yoshua 14:6-14

MAOMBI

(A) MAOMBI DHIDI YA UPOFU WA KIROHO

Asante Yesu kwa kunipa fursa nyingine ya kuomba kuhusiana na hali hii, katika Jina la Yesu.

Eeh Mungu wangu, nisamehe dhambi zangu zote na unihurumie kwa Jina la Yesu Kristo.

Kila miwani za kishetani zinazozuia kupata kuona mambo ya rohoni, nazichoma moto kwa Jina la Yesu Kristo.

Acha moto wa Roho Mtakatifu uondoe kila pazia la uovu lililofunika macho yangu, kwa Jina la Yesu Kristo.

Acha mkono wa Mungu uondoe mtoto wa jicho wa kipepo kutoka katika macho yangu, kwa Jina la Yesu Kristo.

Kila nguvu za asili za kipepo zilizofunga ufunuo wangu wa kiroho, ziondoke sasa kwa Jina la Yesu Kristo.

BWANA, niokoe kutoka katika vifungo vya dhambi na upofu wa kiroho, katika Jina la Yesu Kristo.

Natumia damu ya Yesu Kristo kufungua macho yangu ya roho kwa Jina la Yesu Kristo.

Nguvu zote zilizofunga macho yangu ya kiroho, ziondoke sasa katika Jina la Yesu Kristo.

Kila mwenye nguvu anayesema sitayaona mema ya Mungu katika maisha yangu, akateketezwe katika Jina la Yesu Kristo.

Kila vitu viovu vilivyofanywa katika macho yangu ya kiroho kwa kutumia nguvu za giza, navichoma moto kwa Jina la Yesu.

Kitu chochote katika macho yangu kinachonifanya niende katika mwelekeo usio sahihi, nakifunga na kukirudisha kwa aliyekituma katika Jina la Yesu.

Nayamwagia macho yangu damu ya Yesu na kuyasafisha kwa moto wa Roho Mtakatifu kwa Jina la Yesu Kristo.

Naamuru kila roho ya upofu ipotee kutoka katika maisha yangu katika Jina la Yesu Kristo.

Kila mshale uliorushwa ili kuua macho yangu ya kiroho na kunizuia kutokuona mipango ya uovu dhidi yangu naiondoa katika maisha yangu katika Jina la Yesu Kristo.

Eeh Mungu uokoaye, niokoe kutoka katika upofu wa kiroho na usingizi wa kiroho katika Jina la Yesu Kristo.

Kila nguvu inayotaka kukwanyua macho yangu kutoka katika uso wangu, ife kwa moto wa Roho Mtakatifu na kwa Jina la Yesu Kristo.

Eeh Mungu, fungua macho yangu ya rohoni kuona mahali nguvu zangu zilizofichwa kwa Jina la Yesu Kristo.

BWANA Yesu Kristo, nionyeshe kwa macho ya kiroho mwanaume (au mwanamke) aliye sahihi katika maisha yangu kama mwenzi wangu wa maisha. BWANA Yesu Kristo, nijulishe kama mwanaume (au mwanamke) huyu ni mtu sahihi katika maisha yangu, katika Jina la Yesu Kristo.

Baba yangu, nibatize kwa nguvu ya uwezo wa kuona uwepo wako, katika Jina la Yesu Kristo.

Vikwazo vyovyote kwamba “siwezi kufanikisha chochote katika kufikia hatma ya maisha yangu” naviwasha moto na viungue hata majivu katika Jina la Yesu Kristo.

Nguvu za kichawi zinazotaka nionekane mkongwe mbele za watu, wewe ni muongo, ukasambaratike kwa moto wa Roho Mtakatifu, katika Jina la Yesu Kristo.

Kwa nguvu ya uweza wa Jina la Yesu, napokea uponyaji kutoka katika ukosefu wa shabaha ya maono kwa Jina la Yesu Kristo.

Wewe pazia la giza, sikia Neno la BWANA, anguka chini kwa nguvu ya moto wa Roho Mtakatifu, katika Jina la Yesu.

Nguvu za giza kutoka kwa wachawi zinazoachiwa katika macho yangu ili kunizuia nisifuatilie na kuona kazi zao ovu dhidi yangu, naziwasha moto na kuziua kwa nguvu ya damu na Jina la Yesu Kristo.

(B) MAOMBI KUONDOA PAZIA LA GIZA

Pazia la giza lililofunika kazi za mikono yangu, nakuchoma moto kwa Jina la Yesu Kristo.

Nafunga na kupoozesha kila mwenye nguvu anayeharibu uso wangu kwa Jina la Yesu Kristo.
Kila mkono wa uovu dhidi ya mpango wa Mungu katika maisha yangu, naukausha kwa Jina la Yesu Kristo.

Kila pazia la uovu katika mwili wangu linalosababisha kuharibika kwa mipango yangu, damu ya Yesu Kristo ikaliondoe sasa kwa Jina la Yesu Kristo.

Kila mashambulizi ya kishetani, sikia Neno la BWANA, nakuunguza kwa moto wa Roho Mtakatifu, katika Jina la Yesu Kristo.

Kwa nguvu ya damu ya Yesu Kristo, nafuta kila alama ya karaha katika maisha yangu katika Jina la Yesu Kristo.

Eeh BWANA acha uwezo wako wa kuhuisha nguvu uhuishe maisha yangu kama tai katika Jina la Yesu Kristo.

Najiachilia kutoka katika kila pazia la kipepo la kukataliwa katika Jina la Yesu Kristo.

Eeh Mungu, inuka and uonyeshe maadui zangu kuwa wewe ni Mungu katika maisha yangu kwa Jina la Yesu Kristo.

Nashambulia kwa moto wa Roho Mtakatifu kila muovu anayenichunguza ili kuniua kwa Jina la Yesu Kristo.

Eeh BWANA, inatosha sasa. Acha kila nyoka aliyetumwa kuharibu maisha yangu afutike kwa moto wa Roho Mtakatifu kwa Jina la Yesu Kristo.

Kila utando wa kipepo ndani yangu uondoke sasa na nauunguza kwa moto kwa Jina la Yesu Kristo.

Natangaza uhuru kutoka kila nguvu za giza na ndoto za kipepo katika Jina la Yesu Kristo.

Kila roho ya kishetani na pazia la kipepo linalonifuatilia kunisababishia kukata tamaa, ondoka katika Jina la Yesu Kristo.

Kila nguvu za giza zinazonisababisha nisiwatambue watu walioletwa katika maisha yangu ili kunisaidia na hivyo kufanya nifanikiwe katika maisha yangu, nazitawanya kwa moto wa Roho Mtakatifu katika Jina la Yesu Kristo.

Namdhoofisha kila mtumishi anayetumia nguvu za giza aliyetumiwa ili kuharibu maisha na hatma yangu katika Jina la Yesu kristo.

Kila nguvu ya giza ya chuki katika maisha yangu, natumia damu ya Yesu kujisafisha na kuiondoa kutoka katika maisha yangu katika Jina la Yesu Kristo.

Nakataa kuvaa taswira ya upofu na kuchanganyikiwa katika Jina la Yesu Kristo.

Kwa njia yoyote ile mwanadamu aliyoniwekea vikwazo ili nisioe au kuolewa kwa wakati wa BWANA, kwa rehema zako eeh BWANA, vikwazo hivyo navivunja na eeh BWANA naomba nikapate mwenza wangu wa maisha kwa wakati muafaka na kuweza kupata watoto wa kike na wa kiume katika Jina la Yesu Kristo.

Pazia la kipepo nililorithi kutoka katika ukoo wangu, naliondoa katika maisha yangu katika Jina la Yesu Kristo.

Eeh BWANA, onekana katika hatma yangu na uniumbe upya katika utukufu wako katika Jina la Yesu Kristo.

Kila wingu la giza, linalofunika ndoa yangu na kuifanya isiwe na matunda mema, ondoka katika Jina la Yesu Kristo.

Eeh BWANA, onyesha nguvu yako na uaibishe nguvu zote za giza zinazofikiri zimekamilisha kazi zao juu ya maisha yangu, katika Jina la Yesu Kristo.

Kila nguvu za giza, mapepo, majini na mizimu zilizotumwa kusababisha nikose fursa zangu katika mpango wa Mungu nazisambaratisha katika Jina la Yesu Kristo.

Baba, katika uwepo wa wote wale wanaonisababishia upofu wa kiroho, achilia maisha yangu yakafanikiwe sana na kufikia hatma yangu uliyoikusudia kwenye maisha yangu katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

SIKU YA NANE

TII AGANO LA MUNGU NA KUZIISHI AHADI ZAKE

Wakati wakiwa jangwani, wana wa Israeli hawakumwacha Mungu kwa sababu tu ya hofu lakini pia kutokana na kubweteka na baraka na mafanikio yaliyoyapata. Katika hotuba yake ya kwanza, Musa anaeleza baraka watakazopata wana wa Israeli mara baada ya kuingia katika nchi ya ahadi. Musa anasema kwamba baraka zina uwezekano wa kuzalisha roho ya kubweteka ambayo ni hatari zaidi kuliko kushindwa vitani. ***"Utakapozaa wana, na wana wa wana, mkisha kuwa katika nchi siku nyingi, mkajiharibu na kufanya sanamu ya kuchonga kwa umbo la kitu chochote, mkafanya ambayo ni maovu machoni pa BWANA, Mungu wako, na kumtia hasira; nawashuhudizia mbingu na nchi hivi leo, kwamba karibu mtaangamia kabisa juu ya nchi mwivukiayo Yordani kuimiliki, hamtafanya siku zenu ziwe nyingi juu yake, ila mtaangamizwa kabisa "*** (Kumbukumbu 4:25-26). Hii inaonesha hatari inayoweza kusababishwa na kubweteka kiroho.

Kufuatia mafanikio, watu wanaacha kuwa na kicho cha Mungu na kuanza kuamini kwamba baraka ni haki yao ya kuzaliwa. Badala ya shukrani, tuaanza kujenga hisia ya haki. Siyo vibaya kutafuta baraka, lakini juhudi hizo zinaweza kutujengea kujiingiza katika hatari ya kwenda kinyume na maadili. Ukweli ni kwamba mafanikio tunayoyapata ni mchanganyiko wa ujuzi wetu na bidii katika kazi, ikijumuishwa na mazingira ya bahati na neema ya kawaida ya Mungu.

ISAYA 42:8

MIMI NI BWANA; NDILO JINA LANGU; NA UTUKUFU WANGU SITAMPA MWINGINE, WALA SITAWAPA SANAMU SIFA ZANGU

Mafanikio siyo ya kudumu, na kwa kweli hayakidhi matamanio yetu yote. Mfano mzuri wa ukweli huu unapatikana katika maisha ya Mfalme Uzia. ***"...alisaidiwa mno ajabu, hata akapata nguvu. Lakini alipokuwa na nguvu, moyo wake ulitukuka, hata akafanya maovu, akamwasi BWANA, Mungu wake..."*** (2 Nyakati 26:15-16). Ni kwa Mungu pekee ndipo tunapopata usalama wa kweli na kuridhika (Zaburi 17:15).

Inaweza kukushangaza kwamba matokeo ya kubweteka kiroho siyo kumkana Mungu bali kuabudu sanamu. Musa aliliona hili mapema kwamba watu wakimwacha BWANA watajipa uhuru utakaowafanya kuitumikia "***...miungu, kazi za mikono ya watu, miti na mawe, ambao hawaoni, wala hawasikii, hawali, wala hawanusi"*** (Kumbukumbu 4:28).

Hii maana yake basi nikwamba mafanikio hayapaswi kutufanya tubweteke na kuacha kumtii Mungu na kuacha kufuata maagizo yake. Kama twaweza kukumbuka kuwa neema ya Mungu, Neno lake na muongozo wa Mungu ndio msingi wa mafanikio yetu yote, basi tutaweza kuwa na moyo wa shukrani. Kwa msingi huu, mafanikio na baraka zote tunazozipata zitatumika katika kumtukuza Mungu na kutuletea furaha. Angalizo ni kwamba katika historia, mafanikio yameonekana mara nyingi kuwa chanzo cha uharibifu zaidi kiroho kuliko changamoto tunazopitia. Musa aliwaonya zaidi wana wa Israeli kuhusu hatari ya mafanikio katika Kumbukumbu 8:11-20. Hivyo, inatupasa kutii agano la Mungu na kuziishi ahadi zake ndipo mafanikio na baraka alizotuahidia zitakuwa sehemu ya maisha yetu na zitadumu vizazi hadi vizazi, vinginevyo Mungu atatulaani na tutawarithisha vizazi vyetu laana hizo.

KUTOKA 20:5-6

...KWA MAANA MIMI BWANA, MUNGU WAKO, NI MUNGU MWENYE WIVU; NAWAPATILIZIA WANA MAOVU YA BABA ZAO, HATA KIZAZI CHA TATU NA CHA NNE CHA WANICHUKIAO, NAMI NAWAREHEMU MAELFU ELFU WANIPENDAO, NA KUZISHIKA AMRI ZANGU

Ni kwa kumtii baba yake kwenda kuwapelekea ndugu zake chakula walipokuwa kambini vitani ndiko kulikompelekea Daudi hatimaye kukutana na mafanikio yake ya kumshinda Goliati. Kama Daudi asingelitii na kutekeleza agizo la kutumwa na baba yake angepata wapi ushindi?

> ***"Ndipo Yese akamwambia Daudi mwanawe, Haya! Sasa uwachukulie ndugu zako efa ya bisi, na mikate hii kumi, ipeleke***

> ***upesi kambini kwa ndugu zako; ukampelekee akida wa elfu yao jibini hizi kumi, ukawaangalie, wa hali gani, kisha uniletee jawabu yao."*** (1 Samweli 17:17-18)

Siku zote kutii na kutekeleza kile Mungu anachokisema na kutuagiza kufanya inatuzalishia ushindi na baraka. Daudi, alishinda vita, nakupokea baraka kwa sababu ya utii wake.

Mungu haishii kukuambia utii ila anataka pia uyatunze hayo maagizo yake. Kutunza huku sio kwa maneno, anamaanisha uweke ndani ya moyo wako, usiyasahau maagizo yake muda wote, mahali popote na nyakati zozote, uyakumbuke na uyatende.

Mfalme Sauli alivuliwa ufalme na Mungu kwa kushindwa kwake kuwa mtii na kutekeleza maagizo ambayo Mungu alimuagiza ayafanye.

> "***Naye Samweli akasema, je! Bwana huzipenda sadaka za kuteketezwa na dhabihu sawasawa na kuitii sauti ya Bwana? Angalia, kutii ni bora kuliko dhabihu, na kusikia kuliko mafuta ya beberu. Kwani kuasi ni kama dhambi ya uchawi, na ukaidi ni kama ukafiri na vinyago; kwa kuwa umelikataa neno la Bwana, Yeye naye amekukataa wewe usiwe mfalme."*** (1 Samweli 15:22-23)

Ni muhimu pia kutambua kuwa tunapaswa kutii sauti na maagizo ya Mungu katika hali na mazingira yoyote yale tunayopitia. Usiwe ni mkristo wa kutii sauti ya Mungu ukiwa katika mazingira fulani tu, au kwa muda fulani tu. Mungu anataka muda wote na katika mazingira ya aina yoyote ile umtii; hapo ndipo baraka zake zitakufuata. Katika Kumbukumbu 28:1-14 huoni mahali ambapo Mungu anasema uombe juu ya hizi baraka. Kwa njia nyingine baraka haziombwi, ila wewe ukifuata masharti na vigezo baraka zitakufuata tu, hutasumbuka kuziomba. Na utakapofuata hayo masharti na vigezo ina maana utakuwa umeingia kwenye agano na Mungu na Mungu naye atakutazama tofauti na yule aliye nje ya agano.

MITHALI 4:10-12 (BHN)

MWANANGU, SIKIA NA KUYAPOKEA MANENO YANGU, ILI UPATE KUWA NA MIAKA MINGI YA KUISHI. NIMEKUFUNDISHA NJIA YA HEKIMA, NIMEKUONGOZA KATIKA NJIA NYOFU. UKITEMBEA HATUA ZAKO HAZITAZUIWA, WALA UKIKIMBIA HUTAJIKWAA.

Hebu tuangalie mfano wa baba yetu Ibrahimu ambaye alijikuta ana maagano na Mungu. Katika Mwanzo 12:1-9, Mungu anamwagiza Ibrahimu atoke katika nchi yake, mpaka pale Bwana atakapomwonyesha. Mungu anampa ahadi Ibrahimu kuwa atamfanya taifa kubwa na atambariki kila ambarikie na kumlaani kila amlaaniye. Pamoja na kumuahidi ahadi ya taifa kubwa na ulinzi wa kipekee bado Mungu anampa sharti Ibrahimu atoke katika nchi yake.

Pata picha ni wewe umeshajijenga, una mji mkubwa, mali, una ndugu zako na majirani wazuri, ardhi nzuri na umeishi miaka yote hapo, ghafla leo unaambiwa ondoka na unapokwenda hupajui na hujapata taarifa zake na hujui utasafiri kwa muda gani mpaka huko. Si rahisi kukubali kuondoka; lazima utaanza kwanza kufunga na kuomba ili kumuuliza Mungu au kuijaribu hiyo sauti kama ni ya Mungu au la. Wakati mwingine waweza hata kumbembeleza Mungu akuepushe na hiyo sauti. Lakini kwa kuwa ilikuwa ni ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu na hayo ndio masharti yake ya kufanywa awe taifa kubwa na apewe ulinzi wa kipekee, ilimbidi atii. Na Mungu hakumbariki alipoanza safari, na wala hakumsemesha njiani mpaka alipofika ndipo Mungu anamwambia hapo ndipo.

Hii siyo nyepesi kama unavyo dhania. Ukisoma Mwanzo 13:2 inasema Ibrahimu alikuwa tajiri. Utajiri wa Ibrahimu ulikuja baada ya kutii. Pale alipochukua tu hatua ya kutoka kwao na kwenda mahali Mungu alipomuagiza kwenda hali yake ya uchumi ikabadilika.

Kila unaposoma Neno la Mungu tafuta kwa undani zaidi na kuelewa kile ulichokisoma. Mara nyingi ninapohubiri katika Kanisa letu la Faith Victory International naweka msingi na msisitizo sana katika kusoma, kulifafanua, kulielewa na kulitenda Neno la Mungu. Ili kujua masharti na vigezo unavyotakiwa wewe kuvifuata, na ili uwe na bidii kuvifanya kunahitajika kujifunza Neno la Mungu, siyo kuweka matarajio yako kwenye mafuta na maji, upako na kutolewa vitu kwenye mwili na manabii.

MWANZO 22:18 (BHN)

KUTOKANA NA WAZAWA WAKO MATAIFA YOTE DUNIANI YATABARIKIWA KWA SABABU WEWE UMEITII AMRI YANGU

Unapaswa kutambua pia kwamba unapaswa kusoma Biblia au mistari ya Biblia kwa mapana yake ili kutambua maudhui au muktadha wa andiko unalosoma. Kwa mfano, unaposoma mstari mmoja, huwezi kusimama katika huo tu bila kuelewa maudhui ya kabla na baada ya mstari huo uliousoma. Kuna baadhi ya

mistari ya Biblia haielezi masharti na vigezo moja kwa moja mpaka utakaposoma mistari inayofuatia. Kwa mfano, Kumbukumbu 28:7 inasema;

> ***"BWANA atawafanya adui zako wainukao juu yako kupigwa mbele yako, watakutokea kwa njia moja lakini watakimbia mbele yako kwa njia saba"***

Huu mstari ni mwendelezo wa baraka na ahadi za Mungu kwa wale tu watakao sikia sauti yake na kutunza maagizo yake. Kwa mstari huu wa 7, lazima utafute maagizo yake ya nini ufanye ili maadui wainukao juu yako waweze kupigwa na BWANA. Ni rahisi kuanza kuwalaani adui zako na kuwaombea wafe, lakini je ndivyo Mungu asemavyo juu ya adui zako, aliposema watakimbia kwa njia saba ina maana unatakiwa uombe wakimbie? Mstari huu lazima usomwe na Warumi 12:19

> ***"Wapenzi msijilipize kisasi, bali ipisheni ghadhabu ya Mungu, maana imeandikwa kisasi ni juu yangu mimi...."***

Je, kwa mstari huu unapaswa umkumbushe Mungu atulipizie kisasi? Maana yeye ndio mwenye uwezo na mamlaka ya kutulipia kisasi. Bado tunahitaji kuchunguza maandiko mengine juu ya adui zetu. Mathayo 5:43-44 inasema;

> ***"mmesikia kwamba imenenwa umpende jirani yako na umchukie adui yako; lakini mimi nawaambia wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi"***

Yesu anataka tuwapende adui zetu na tuwaombee. Sasa ili adui zako waliokuja kwa njia moja watoke kwa njia saba huna budi kuwapenda na kuwaombea. Hiyo ndio kazi yako. Halafu suala la kisasi na ghadhabu na kuwafukuza, na kuwaua si lako ni la Mungu. Kwa maana nyingine basi, kigezo cha utekelezaji wa Kumbukumbu 28:7 ni kwa kumpenda adui yako na kumwombea. Namna adui yako atakavyotoka kwako ni kazi ya Mungu ndiye anayefanya. Kumwombea adui haina maana uombe atoke, ina maana uombe mema yamkute si mabaya maana umpendaye huwezi kumwombea apatwe na mabaya.

Hii ni mifano michache tu itakayokufanya uweze kuzichunguza ahadi za Mungu na kuzifuatilia kwa bidii na kuyatenda na kuyatii masharti na maagizo yake. Usijaribu kumlazimisha Mungu atimize ahadi zake kwako wakati wewe hujaingia

kwenye agano naye kuyatimiza ya kwake, yaani hufuati masharti na vigezo vitakavyomfanya Mungu atimize ahadi zake kwako.

Usitafute Njia za Mkato

Wengi wetu tunataka njia za mkato ili Mungu atimize ahadi zake. Wengi tunataka tuombewe kwa muda mrefu na kwa kufunga sana tukidhani Mungu ndipo atatimiza ahadi yake. Napenda nikuambie tu kwamba sahau, maana Mungu ni Mungu wa taratibu na kanuni. Fuata masharti na kanuni zake naye atatimiza. Kwa kusema hivi simaanishi kwamba usiombe, la hasha. Maombi ni muhimu sana lakini fanya maombi na jiulize unakidhi masharti na vigezo vya hiyo ahadi unayoomba itimie kwako? Unaweza kufunga sana ila matokeo yakawa hayapo. Ni vyema ukafunga na kuomba, lakini usisahau kufuata kanuni, taratibu na maagizo ya Mungu ili uweze kufanikiwa kwa kile unachoombea.

Kwa mfano, katika Mathayo 20:20-23 inasema;

> ***"Ndipo mama yao wana wa Zebedayo akamwendea pamoja na wanawe akamsujudia, na kumwomba neno. Akamwambia, wataka nini? Akamwambia, agiza kwamba hawa wanangu wawili waketi mmoja mkono wako wa kuume na mmoja mkono wako wa kushoto, katika ufalme wako. Yesu akajibu akasema hamjui mnaloliomba..... lakini kuketi mkono wangu wa kuume na mkono wangu wa kushoto, sina amri kuwapa, bali watapewa waliowekewa tayari na Baba yangu"***

Ina maana huyu mama alipenda sana wanawe waketi katika ufalme wa Yesu. Alitumia njia ya mkato kwa kuomba kuwa Yesu aamuru hivyo. Naye Yesu anamwambia wazi hujui uliombalo maana Yesu alikwisha wafundisha kuwa kwenda kwa Baba ni kujikana na kuubeba msalaba wako mwenyewe. Badala ya kuomba nguvu na uwezo juu ya wanawe ili waweze kila mmoja kujikana na kubeba msalaba wao, yeye anataka njia ya mkato.

Ndivyo tulivyo wengi wetu, hatuna utofauti na mama huyu. Hatutaki kutii maagizo ila tunapenda njia za mkato. Tusidanganyike Mungu hatendi nje ya kanuni zake.

Mungu hujibu Maombi Ili Kutimiza Neno (Agano) Lake

Ukiwa na bidii ya kusikia na kutunza maagizo ya Mungu, kuna mambo Mungu atakutendea ambayo hayajatokana na maombi yako bali kwa utii wako Mungu atakutendea tu. Kutoka 6:4-5 inasema:

> ***"Tena nimelithibitisha agano langu nao kuwapa nchi ya Kanani nchi ya kukaa kwao hali ya ugeni. Na zaidi ya hayo nimesikia kuugua kwao wana wa Israeli, ambao wamisri wanawatumikisha nami nimelikumbuka agano langu..."***

Pamoja na wana wa Israeli kuomba na kuugua kwa ajili ya mateso waliyoyapata toka kwa Wamisri lakini Mungu hakuwajibu maombi yao. Maombi ya Waisraeli yalimkumbusha Mungu pale tu ahadi yake kwa Ibrahimu ilipo timia. Mungu hakujibu maombi yao bali alichofanya ni kutimiza ahadi yake na agano aliloingia na Ibrahimu. Maana alimwahidi Ibrahimu kuwa atakuwa na uzao mkubwa na huo uzao utakaa ugenini miaka mia nne (Mwanzo 15:13-14). Ibrahimu alitimiza ahadi yake kwa Mungu akafariki, ila uzao wake ukaenda ugenini, likabaki agano la kukaa ugenini kwa wana wa Israeli kwa muda wa miaka mia nne. Israeli wakaendelea kuzaliana huko Misri na hakuna aliyekumbuka kurudi Kanani, mpaka miaka mia nne ilipotimia ndipo Israeli wakashtuka na kuanza kuugua na kumlilia Mungu. Mungu naye hakuwatoa Misri eti kwa kuwa wameomba sana au wameugua sana, Hapana! Aliwatoa tu kwa sababu alikumbuka alichoagana na Ibrahimu. Kutoka kwa wana wa Israeli Misri kwenda Kanani hayakuwa matokeo ya maombi yao; walitoka sababu ya agano la Mungu na Ibrahimu.

LUKA 1:45 (BHN)

HERI YAKO WEWE ULIYESADIKI KWAMBA YATATIMIA YALE BWANA ALIYOKUAMBIA

Ukiingia kwenye agano na Mungu uwe na uhakika hilo agano husika Mungu atalilinda vizazi hata vizazi. Wewe utapita lakini uzao wako utalindwa kwa mujibu wa agano ulililoingia na Mungu wako. Maana ndivyo isemavyo Zaburi 105:7-8

> ***"Yeye Bwana ndiye Mungu wetu duniani mwote mna hukumu zake, analikumbuka agano lake milele, neno lile alililoliamuru vizazi elfu"***

Unachopaswa ni wewe kung'ang'ania kufuata maagizo yake tena kwa bidii ukiwa bado u hai, na Mungu hatakuacha wewe wala uzao wako. Maana Ibrahimu alikufa akiwa ameacha mtoto wa ahadi mmoja Isaka, lakini kupitia ahadi ya Mungu na

Ibrahimu, makabila kumi na mawili ya Israeli yalitokea. Hata sisi pia ni uzao wa Ibrahimu na tunarithi baraka hizo kwa kuzaliwa upya kupitia kumpokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wa maisha yetu. Japo Israeli wanamuudhi na kumtenda Mungu dhambi, lakini ile mbegu aliyoipanda Ibrahimu ya utiifu wa agano la Mungu ndio inayoifanya Israeli ya leo iwe taifa teule mbele za Mungu. Yote hii ni nguvu ya agano la Mungu na Ibrahimu.

Ukiangalia maisha ya wakristo wengi kiuchumi yana changamoto nyingi. Hii ni kwa sababu hawapendi kufuata maagizo ya Mungu ili waweze kubarikiwa kiuchumi. Wakristo wengi wanajua kabisa masharti ya agano la uchumi ni pamoja na kumtolea Mungu zaka, sadaka, dhabihu na matoleo mengine. Lakini wao ni wachungu na wachoyo mno kutoa, wamejionea huruma kiasi cha kushindwa kumtolea Mungu. Malaki 3:10-12 inasema:

> ***leteni zaka kamili ghalani, ... Asema BWANA wa majeshi, mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagia baraka hata isiwepo nafasi ya kutosha au la"***

Huu ni mstari mmoja tu kati ya mingi ihusuyo uchumi, na Mungu anataka zaka kamili sio nusu nusu. Ninachotaka kusisitiza hapa ni kuhusu utii wa agano la Mungu kuhusu jambo unalotaka litimizwe kwako na Mungu. Kila ahadi inapaswa kushughulikiwa kivyake na sio kuchanganywa. Kumbuka kuwa huwezi kushinda yote hayo bila kuingia agano na Mungu, na kama kuna roho zinazokuzuia usiingie agano hilo na Mungu basi ni muda mzuri wa kumshughulikia Goliati wako ili akupishe uende kwenye mafanikio yako nawe uwe mshindi.

ANDIKO LA KUSIMAMIA

Yeremia 1:12
Zaburi 138:2

MAOMBI

YESU Mwana-kondoo wa Mungu, Jina lako ni la thamani sana. Nakuinua na kulibariki Jina lako Takatifu. Baba, wewe ni kila kitu kwangu. Bila wewe, siwezi kufanya lolote. Wewe ni Mfalme wangu, mtawala wa kila kitu na hakuna anayeweza kulinganishwa na wewe. Wewe ni shauku ya moyo wangu, Eeh Bwana. Nakupa moyo wangu, mwili wangu na nafsi yangu.

Nataka nizame katika uwepo wako kwa namna ambayo sitaelewa hata kinachotokea. Nina njaa na kiu nawe. Uwe kiongozi wangu, Eeeh BWANA na unisaidie kulitii Neno lako. Wasaidie wale wasiokutii ili wautafute uso wako, Eeh BWANA na uwasamehe kwa maana hawajui wanalolifanya. Nipe hekima pale ninapokosa ufahamu, ili nitambue namna bora ya kukuamini na kukutii.

Baba,

Wewe ni Baba mwema. Haubadiliki, haunichoki kamwe, wala kukata tamaa ya kunisaidia. Ikiwa Neno lako linasema kwamba wewe unanijali, basi nachagua kuamini katika Neno lako kwamba unanijali na kunitakia yaliyo mema. Nautua mzigo wote ninaoubeba katika mikono yako iliyo salama [taja mizigo (changamoto zote) yote uliyobeba kadri utakavyokumbuka].

Nakabidhi nafsi yangu chini ya ulinzi wako. Sitakuwa na hofu tena. Nakataa kuhofu, kwa sababu Baba yangu wa Mbinguni ananijali na anatambua kila changamoto ninayopitia leo. Sitakata tamaa na sitaondolewa katika imani hii kwa BWANA Yesu. Nitasimama kwa ujasiri na kumtangaza Mungu kwamba yu mwema. Unanijali, na kwa sababu hiyo naweza kuishi maisha yasiyokuwa na hofu, nikipuuzia michanganyiko yote ya kidunia inayoletwa na yule adui wa nafsi yangu anayenitaabisha.

Asante BWANA wangu na Mungu wangu kwa upendo wako kwangu, ambao ndio muhimu katika maisha yangu. Nifundishe namna bora ya kukutumainia, kukuamini na kukutii zaidi na zaidi kila siku.

Katika Jina la Yesu Kristo, Amina.

SIKU YA TISA

SONGA MBELE KWA USHINDI

Mwisho wa simulizi ya Daudi na Goliati, tunasoma ***"Hivyo Daudi akamshinda yule Mfilisti kwa kombeo na jiwe, akampiga Mfilisti, akamwua; walakini Daudi hakuwa na upanga mkononi mwake"*** (1Samuel 17:50). Kwa muda wa masaa kadhaa, kijana mchunga mifugo akiwa tu na kombeo na imani katika Mungu akaliua lile jitu lililoogopewa sana lililokuwa likidhihaki jeshi la Waisraeli kwa muda wa siku arobaini. Mchungaji wako, Yesu Kristo, atafanya vivyo hivyo katika maisha yako kama ukimruhusu (angalia Yohana 10:11).

Katika Zaburi 23:5 Daudi anamzungumzia BWANA ***"Waandaa meza mbele yangu, machoni pa watesi wangu, umenipaka mafuta kichwani pangu, na kikombe changu kinafurika."*** Yesu Kristo, Mwokozi wako, ameahidi kukuongoza na kukulinda, si kwa kutokuwepo adui zako, lakini mbele zao. Kwa kadri shinikizo, giza na vita katika maisha haya vinapokusonga, Mchungaji wako analeta karamu ya mahitaji yako yote mbele ya maadui zako. Anakupa yote unayoyahitaji si tu ili uweze kukombolewa lakini uweze kustawi katika uhuru ulioupata kupitia Yesu Kristo.

Biblia inasema kwamba Yesu si tu kwamba ni Mungu wako Mchungaji, lakini pia ni Simba wa kabila la Yuda (angalia Ufunuo wa Yohana 5:5). Mngurumo wake unatawala mataifa. Sauti yake inamwangamiza adui. Lakini kwa kitambo kifupi, shetani ameruhusiwa kutembea na kutafuta nyufa, ambapo kwa kupitia hizo anaweza kuingia katika akili yako. Usipomsimamisha, basi atakuwa ndiye

anayekaa katika meza. Na akikaa katika meza yako, kazi anayoifanya ni kuondoa tumaini lako kwa Mungu. Atajaribu kukuambia kuwa uko mpweke, mwenyewe katika vita na huna nafasi ya kushinda maadui zako.

MITHALI 19:21

MNA HILA NYINGI MOYONI MWA MTU; LAKINI SHAURI LA BWANA NDILO LITAKALOSIMAMA

Kwa kipindi kama hicho unapaswa kukubaliana na Daudi, ambaye, pamoja na kushuhudia upinzani mkubwa dhidi yake, aliweza, kwa ujasiri mkubwa kusema ***"naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya, kwa maana Wewe uko pamoja nami"*** (Zaburi 23:4). Daudi alifahamu Mungu alikuwa na udhibiti wa kila jambo. Alitambua kuwa katika wakati mgumu na giza nene Mungu alikuwa upande wake, akitembea naye na kumwongoza katika bonde. Unaweza pia kuwa na tumaini hilo, lakini tu kama ukikataa kumwacha yule adui akae katika meza yako.

Hii ni kwa sababu kama adui yuko mezani pako, atajaribu kukushawishi kuwa hutaweza. Atahakikisha anaweka mawazo hasi ndani ya kichwa chako. Atajaribu kukushawishi kuwa kuna jambo jema katika meza nyingine ambayo Mungu hajakusudia wala siyo mpango wake uifikie. Badala yake unapaswa kuchagua kuamini kwamba Mchungaji wako ameahidi kukuongoza kupita katika bonde, kwamba daima atakuwa nawe, kwamba anajua kilicho bora kwa ajili yako, na kwamba wewe ni mwanawe mpendwa.

Hivyo leo, chukua kiti chako mbele ya meza nzuri ya Mungu. Kaa chini, uwe mtulivu na ufurahie uwepo wa Mungu wako wa mbinguni. Nenda kwake kila wakati unapoona umechoka na kulemewa na mizigo mizito, kwa sababu ameahidi kukupumzisha (Mathayo 11:28). Usiweke msisitizo wala kuzingatia maadui zako wanaokuzunguka, bali zaidi kwa kufahamu kuwa Mungu yupo kwa ajili yako. Songa mbele kwa ushindi aliokwisha kukupatia na shuhudia namna mmoja baada ya mwingine wa maadui zako wakiangushwa.

ANDIKO LA KUSIMAMIA

Zaburi 23 :1
Zaburi 23 :4-5

MAOMBI

BWANA, nakuja kwako leo na nakushukuru kwa ushindi katika maisha yangu ambao nimekwisha shinda dhidi ya adui zangu. Asante Yesu Kristo kwamba ulinipenda hata ukautoa uhai wako kwa ajili yangu ili niweze kupata wokovu. Asante Mungu kwa sababu daima uko upande wangu. Ninapaswa tu kutambua na kuutangaza ushindi wako katika maisha yangu.

Ukweli huu unanipa faraja, starehe, mapumziko na uponyaji katika roho yangu. Kwa sababu yako, sipaswi kuwa na hofu dhidi ya mipango ya adui zangu. Kama uko upande wangu ni nani aliye juu yangu? Nionyeshe ninachopaswa kuona kuhusu ushindi katika maisha yangu. Nionyeshe wakati na namna gani ya kuomba kwani ninalindwa chini ya mikono yako.

Katika Jina la Yesu Kristo, Amina.

Zaburi 56:9 ***"Ndipo adui zangu watarudi nyuma siku ile niitapo. Neno hili najua kuwa MUNGU yu upande wangu."***

1 Wakorintho 15:57 ***Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa BWANA wetu Yesu Kristo.***

Mungu Baba, nakushukuru na kukusifu kwa sababu ninao ushindi kupitia BWANA wetu Yesu Kristo.

Zaburi 40:14-15 ***Waaibike, wafedheheke pamoja, wanaoitafuta nafsi yangu waiangamize. Warudishwe nyuma, watahayarishwe, wapendezwao na shari yangu. Wakae hali ya ukiwa, na iwe aibu yao, wanaoniambia, Ewe! Ewe!***

Wale wote wanaotaka kuharibu maisha yangu wakaaibishwe na kufedheheshwa; wale wote wanaotamani uharibifu wangu wakarudishwe nyuma kwa aibu katika Jina la Yesu Kristo. Uwachanganye. Ukawarejeshe walikotoka na kuwatawanya – wale wote wanaotaka kuniangamiza. Waaibishe wote hawa wenye mizaa na wakashindwe kabisa.

Zaburi 35:4 ***Waaibishwe, wafedheheshwe, wanaoitafuta nafsi yangu. Warudishwe nyuma, wafadhaishwe, wanaonizulia mabaya***

Eeh BWANA Mungu wangu, naomba wale wote wanaoyatafuta maisha yangu waaibishwe na kufedheheshwa. Wale wote wanaopanga njama dhidi ya maisha yangu wakarudishwe nyuma na kusikitishwa katika Jina la Yesu.

Eeh BWANA Mungu wangu, waaibishe wale wote wanaojaribu kuniua (kimwili au kiroho). Warejeshe nyuma na kuwachanganya katika Jina la Yesu.

Zaburi 35:26 ***Waaibishwe, wafedheheshwe pamoja, wanaoifurahia hali yangu mbaya. Wavikwe aibu na fedheha, wanaojikuza juu yangu***.

Eeh BWANA Mungu wangu, wale wote wanaofurahia kuumizwa kwangu waaibishwe na wakachanganyikiwe. Wakavishwe mavazi ya aibu kwa kuwa wamenichimbia kaburi na kunitakia aibu katika maisha yangu.

Zaburi 70:2 ***Waaibike, wafedheheke, wanaoitafuta nafsi yangu. Warudishwe nyuma, watahayarishwe, wapendezwao na shari yangu.***

Eeh Mungu, Baba yangu, wale wote wanaoitafuta roho yangu wakaaibishwe na kufedheheshwa. Wale wote wanaotaka nipate aibu wakarejeshwe nyuma na kuchanganyikiwa kwa Jina la Yesu.

BWANA Mungu wangu, wale wote wanaonyemelea maisha yangu na wanaofurahia katika matatizo yangu, wakachanganyikiwe na uwaaibishe ili furaha yao ikomeshwe. Usiwaruhusu waendelee kunikejeli na kunikomoa. Wale wote wanaotaka kuniua kiroho au kimwili ukawaaibishe na kuwafarakanisha. Wakarejeshwe nyuma na kuaibishwa katika Jina la Yesu Kristo.

Zaburi 31:17 ***Ee BWANA, nisiaibishwe, maana nimekuita, waaibishwe wasio haki, wanyamaze kuzimuni.***

BWANA Mungu wangu, naomba nisiaibishwe kwa sababu nimeliitia Jina lako takatifu. Waache waovu wote waaibishwe na kunyamazishwa katika makaburi yao katika Jina la Yesu

Zaburi 31:18 ***Midomo ya uongo iwe na ububu, imneneayo mwenye haki maneno ya kiburi, kwa majivuno na dharau.***

BWANA Mungu wangu, acha midomo inenayo ubaya na uongo na kusema

maneno ya ukatili kwa kujigamba na kuwadharau wenye haki, wakaaibishwe na kunyamazishwa.

BWANA Mungu wangu, acha midomo inenayo ubaya na uongo inyamazishwe kabisa. Acha midomo ya wenye kiburi wanaowashitaki wenye haki kwa matendo mabaya wakanyamazishwe katika Jina la Yesu Kristo.

Yeremia 20:11-12 ***Lakini BWANA yu pamoja nami, mfano wa shujaa mwenye kutisha; kwa hiyo hao wanaonionea watajikwaa, wala hawatashinda; watatahayarika sana. Kwa sababu hawakutenda kwa akili, wataona aibu ya milele, ambayo haitasahauliwa kamwe. Lakin Ee BWANA wa majeshi, wewe wawajaribu wenye haki, waona viuno na mioyo, nijalie kuona kisasi chako juu yao; kwa maana nimekufunulia wewe neno langu.***

Eeh BWANA, Mungu wangu, uwe pamoja nami kama shujaa mwenye nguvu atishaye. Watesaji wangu wakaangushwe na kukata tamaa. Kamwe wasinishinde wala kufanikiwa. Wakapatwe na aibu kubwa na wakapate machafuko ya milele, katika Jina la Yesu Kristo.

Isaya 54:17 ***Kila silaha itakayofanyika juu yako haitafanikiwa na kila ulimi utakaoinuka juu yako katika hukumu utauhukumu kuwa mkosa. Huu ndio urithi wa watumishi wa BWANA, na haki yao inayotoka kwangu mimi, asema BWANA.***

Eeh Bwana, pasiwepo na silaha itakayofanyika juu yangu itakayofanikiwa. Kila ulimi utakaoinuka dhidi yangu katika hukumu wewe eeh Mungu ukauhukumu kuwa mkosa katika Jina la BWANA wetu Yesu Kristo.

Amina

HITIMISHO

MAOMBI YA VITA VYA KIROHO

"Heri mtu astahimiliye majaribu; kwa sababu akiisha kukubaliwa ataipokea taji ya uzima, Bwana aliyowaahidia wampendao."
– Yakobo 1:12

Umuhimu wa Kupigana Vita vya Kiroho Kila Wakati Kupitia Maombi

Katika Mwanzo 17:11-12 Neno la Mungu linasema:

> *"Ikawa, Musa alipouinua mkono wake, Israeli walishinda; na alipoushusha mkono wake, Amaleki walishinda. Lakini mikono ya Musa ilikuwa mizito; basi wakatwaa jiwe, wakaliweka chini yake akalikalia. Haruni na Huri wakaitegemeza mikono yake, mmoja upande huu na mmoja upande huu; mikono yake ikathibitika hata jua lilipokuchwa. Yoshua akawaangamiza Amaleki na watu wake kwa ukali wa upanga."*

Biblia inatuambia kwamba, wakati Yoshua alipokuwa mstari wa mbele bondeni akipigana na Waamaleki, Musa alikuwa juu kileleni (kwenye mlima). Alipokuwa akiinua mikono yake, Yoshua aliyekuwa kwenye mstari wa mbele vitani alishinda, lakini alipoishusha mikono yake, Yoshua alishindwa vita. Kumbuka kwamba Musa hakushusha mikono yake kwa chaguo lake, isipokuwa ilikuwa kwa sababu ya uchovu. Lakini adui hakujali sababu ya uchovu, yeye alishinda kupitia uchovu huo wa Musa.

Kwa sababu hiyo, mbinu pekee aliyotumia Musa kuhakikisha Yoshua anashinda

katika uwanja wa vita ilikuwa ni kuwaomba Haruni na Huri wamtegemeze mikono yake ili iendelee kuinuliwa na hivyo kuwezesha ushindi wa wana wa Israeli kupitia Yoshua.

Maisha yako yanapitia misimu miwili; Musa katika kilele cha mlima na Yoshua bondeni. Ni mambo unayoyafanya katika maombi na yale uyafanyayo katika shughuli zako za kila siku (iwe kazini, kwenye biashara, ndoa, huduma na chochote ukifanyacho kukupatia kipato).

Kila ukifanyacho katika maombi na shughuli zako zingine zina muunganiko. Kila wakati maisha yako ya maombi yanapokuwa duni, maadili yako na hata maisha yako ya kiroho yanakuwa duni pia. Na hii inapelekea pia maeneo mengine ya maisha yako kuanza kukosa afya (kuwa duni) kila mara maisha yako ya maombi yanapokuwa duni pia.

Kwa msingi huo huo, tukiwa akina Musa na Haruni na Huri wa leo, tusiache kuinua mikono yetu katika maombi kwa sababu tu maisha yetu yamebarikiwa; tumefanikiwa na kujibiwa kile tulichokuwa tukiomba; au tumechoka sana; au tumetingwa na shughuli nyingi za kimaisha. Kwa sababu yoyote ile, tusiache kuomba, kwa sababu athari yake itatugharimu sana katika eneo la vita vya kiroho.

Kumbuka kwamba kila wakati unapokuwa katika maombi, unamfanya shetani akose nguvu na uweza wa kupambana nawe na kukushinda. Ni katika maombi tu ndipo unapopata nguvu kupitia Roho Mtakatifu ya kushinda kazi zote za mwili, ambazo kupitia hizo adui huzitumia kutushinda. Ndio maana shetani atatumia mbinu zote kukuzuia usiombe kwa sababu anajua nguvu iliyopo katika maombi yako.

Kupambana Vita

Tunahitaji nyenzo katika vita vya kiroho pia. Kwa sababu hiyo, tutaeleza kwa ufupi katika kipengele hiki kukuelekeza kwa vitendo, na kukupa taarifa sahihi na ufahamu namna gani ya kupigana na kushinda vita ya kiroho.

Ulimwengu, mwili na ibilisi wataendelea kushindwa kama tutatumia silaha za vita vyetu. BWANA wetu Yesu Kristo ametupatia zana au nyenzo tunazohitaji kwa ajili ya vita hivyo. BWANA wetu Yesu Kristo amekwisha shinda vita hivyo kwa niaba yetu hata kabla hatujapigana. Alitumia zana hizo ambazo ametupatia

ili kushinda vita hivi. Ushindi wake ni ushindi wetu pia.

Kwa maana hiyo basi, ni jukumu letu kutumia nyenzo hizo ambazo tumepewa na Yesu Kristo kwa rehema na neema yake. Kila wakati unapozitumia utamshukuru Mungu kwa zana za ushindi alizotupatia. Kama vile kwa fundi seremala anavyomshukuru mtu aliyempatia boksi lenye zana zote za ufundi kwa ajili ya kazi yake, ndivyo pia utakavyomshukuru sana Mungu kwa kukupa zana za kupigana na kuvishinda vita vya kiroho.

Kama tunavyoona katika Biblia, Mungu ni mwenye nguvu na uweza katika kutushindia vita dhidi ya adui zetu. Ukweli huu lazima uzame sana ndani ya roho na nafsi zetu. Na ukweli huu utafanyika kuwa sehemu ya maisha yetu kama tutapata uelewa wa Neno Takatifu la Mungu na hatimaye kulitumia Neno hilo hima katika maisha yetu.

Kwa maana hiyo basi, tunapaswa kila siku kuikiri imani yetu katika Yesu Kristo BWANA wetu, kama kitu muhimu sana katika kuishinda vita ya kiroho tunayopigana kila siku. Huu ndio msingi wa kwanza kabisa wa kiroho ambao utakupa uweza wa ushindi kila siku dhidi ya adui zako. Soma Neno la Mungu kila siku kwa ajili ya kukuelimisha na kukujenga katika imani.

Ukiri wa Imani Kila Siku

“Leo nimeamua kwa makusudi kuchagua kujisalimisha binafsi kwa Mungu kama alivyojidhihirisha kwangu kupitia Neno lake Takatifu ambalo kwa uaminifu nalikubali kama pekee ndilo lililovuviwa, lisilotetereka na lenye mamlaka na majibu katika maisha ya kila siku ya mwanadamu. Siku ya leo sitamhukumu Mungu wala kazi Yake wala sitajihukumu mwenyewe na kuwahukumu wengine kwa sababu ya fikra na hisia zangu.

Natambua kwa imani kwamba Utatu Mtakatifu wa Mungu unastahili heshima, kutukuzwa na kuabudiwa kama Muumbaji, Mpaji na mwisho wa vitu vyote. Nakiri kwamba Mungu, Muumbaji wangu, aliniumba kwa ajili yake Mwenyewe. Kwa sababu hiyo, siku ya leo, nachagua kuishi kwa ajili Yake pekee (Ufunuo 5:9,10; Isaya 43:1,7,21; Ufunuo 4:11).

Natambua kuwa kwa imani Mungu alinipenda na kunichagua kupitia Yesu Kristo hata kabla ya ulimwengu haujaumbwa (Waefeso 1:1-7).

Natambua kwa imani kwamba Mungu amethibitisha upendo wake kwangu kwa kumtuma mwanae pekee Yesu Kristo kufa badala yangu, ambaye katika Yeye kila jambo limekwisha fanyika kwa ajili ya maisha yangu yaliyopita, ya sasa na ya baadaye kwa kazi yake ya msalaba na kwamba nimeuhishwa, nimepandishwa na kuketishwa pamoja na Yesu Kristo mahali patakatifu na kutiwa mafuta ya Roho Mtakatifu (Warumi 5:6-11; Warumi 8:28; Wafilipi 1:6; Wafilipi 4:6,7,13,19; Waefeso 1:3; Waefeso 2:5,6 na Matendo 2:1-4, 33).

Natambua kwa imani kwamba Mungu amenipokea kama mwanae kwa sababu nimempokea Yesu Kristo kama BWANA na Mwokozi wangu (Yohana 1:12; Waefeso 1:6); kwamba amenisamehe (Waefeso 1:7); ameniasili katika familia yake, na kuchukua majukumu yote kwa niaba yangu (Yohana 17:11, 17; Waefeso 1:5; Wafilipi 1:6); amenipa uzima wa milele (Yohana 3:36; 1 Yohana 5:9-13); ametumia haki kamilifu ya Kristo kwangu ili kwamba nihesabiwe haki (Warumi 5:1; Warumi 8:3,4; Warumi 10:4); amenikamilisha ndani ya Kristo (Wakolosai 2:10); na amejitoa Mwenyewe kwangu kama utoshelevu wangu wa kila siku kupitia maombi na maamuzi ya kiimani (1 Wakorintho 1:30; Wakolosai 1:27; Wagalatia 2:20; Yohana 14:13, 14; Mathayo 21:22; Warumi 6:1-19; Waebrania 4:1-3,11).

Natambua kwa imani kwamba Roho Mtakatifu amenibatiza kuwa katika mwili wa Kristo (1 Wakorintho 12:13); na ameniweka muhuri (Waefeso 1:13,14); amenipaka mafuta kwa maisha na utumishi (Matendo 1:8; Yohana 7:37-39); ananiongoza kwenye maisha ya ushirika wa ndani kabisa na Yesu Kristo (Yohana 14:16-18; Yohana 15:26,27; Yohana 16:13-15; Warumi 8:11-16); na amejaa ndani ya maisha yangu (Waefeso 5:18).

Natambua kwa imani kwamba ni Mungu pekee anayeweza kushughulika na dhambi na ni Mungu pekee ndiye awezaye kuleta utakatifu katika maisha. Nakiri kwamba katika wokovu wangu, sehemu yangu ilikuwa tu kumpokea Yeye na kwamba alishughulika na dhambi zangu na kuniokoa. Sasa nakiri kwamba ili niishi maisha ya utakatifu, naweza tu kujisalimisha tu kwenye mapenzi Yake na kumpokea kama utakaso wangu; nikimuamini Yeye kufanya lolote katika maisha yangu, ndani na nje, ili niwezeshwe kuishi maisha ya utakatifu, uhuru, utulivu na nguvu kwa utukufu wa Mungu (Yohana 1:12; 1 Wakorintho 1:30; 2 Wakorintho 9:8; Wagalatia 2:20; Waebrania 4:9; 1 Yohana 5:4; Yuda 24).

Baada ya ukiri kwamba Mungu anastahili kusifiwa, na kwamba Neno la Mungu ndilo lenye mamlaka kwenye kila eneo la maisha ya mwanadamu, kwamba

Mungu anaweza kushughulika na dhambi na kuachilia maisha ya utakatifu, natambua tena utegemezi wangu wote kwake Mungu na najisalimisha kwake pekee. Nakubali ukweli kwamba kuomba kwa imani ni lazima kabisa ili nifikie mapenzi na rehema za Mungu katika maisha yangu ya kila siku.

Natambua kwamba imani ni kumuamini Mungu kabisa na kupitia huko, Mungu ametoa riziki zetu za kila siku. Kwa sababu hiyo basi, nafanya maamuzi yafuatayo kwa imani:

1. Leo (Hesabu 3:6, 13, 15; 4:7) nafanya maamuzi ya imani ya kujisalimisha kabisa kwenye mamlaka ya Mungu kama ajidhihirishavyo katika Maandiko Matakatifu kumtii. Natubu dhambi zangu zote, na kukiri ukweli wa maisha yangu ya dhambi katika asili yangu ya zamani, na kwa kumaanisha kabisa naamua kutembea katika nuru, pamoja na Kristo, katika kila saa ya siku ya leo (Warumi 6:16-20; Wafilipi 2:12, 13; I Yohana 1:7, 9).

2. Leo naamua kwa imani kujisalimisha kabisa kwenye mamlaka ya Mungu kama yalivyodhihirishwa katika Maandiko Matakatifu – kumuamini Mungu. Nalikubali tu Neno lake kama mamlaka iliyojitosheleza. Sasa naamini kwamba kwa sababu nimekiri na kutubu dhambi zangu zote, amenisamehe na kunisafisha (I Yohana 1:9). Nakubali Neno lake la ahadi kuwa limenitosheleza na kunipa utulivu, na nitafanya sawasawa na Neno la Mungu linavyonielekeza (Kutoka 33:1; 1 Wakorintho 1:30; 2 Wakorintho 9:8; Wafilipi 4:19).

3. Leo nafanya uamuzi wa imani kutambua kwamba Mungu ametengeneza mazingira yote yanayoniwezesha kutimiza mapenzi yake na wito wake kwangu. Kwa sababu hiyo basi, sitatoa visingizio vyovyote vile kwa ajili ya dhambi zangu na kushindwa kwangu (1 Wathesalonike 5:24).

4. Leo nafanya uamuzi wa imani kwa kukusudia kupokea kutoka kwa Mungu kila alilonilandalia. Nakana kila juhudi zangu binafsi ili niishi maisha ya Kikristo na kutenda mapenzi ya Mungu; nakana maombi na mafundisho potofu kwamba Mungu abadilishe mazingira na watu ili kuniwezesha niishi maisha ya utakatifu; nakana mafundisho potofu kuhusu Roho Mtakatifu na nakana dhamira, nia, malengo na kazi potofu ambazo ni kinyume cha Biblia zinazokusudia kuendeleza kiburi cha dhambi.

a. Sasa nampokea kwa dhati Yesu Kristo kama utakaso wangu na uweza wa kunisafisha kutoka utu wangu wa zamani; na namuomba Roho Mtakatifu akamilishe ile kazi ya Kristo ya msalaba katika maisha yangu. Nikishirikiana na kumtegemea Yeye, natii amri yake ya "kuuvua utu wa kale" (Warumi 6:1-14; 1 Wakorintho 1:30; Wagalatia 6:14; Waefeso 4:22).

b. Sasa nampokea kwa dhati Yesu Kristo kama utakaso wangu na hasa kuwa uwezesho wangu kila wakati kuishi maisha ya bila dhambi na namuomba Roho Mtakatifu aniwezeshe kuikamilisha kazi ya ufufuo wa Kristo ili niishi maisha mapya ya wokovu. Nakiri kuwa Mungu pekee ndiye awezaye kushughulika na dhambi zangu na kwamba ni Mungu pekee ndiye awezaye kunipa utakatifu na tunda la Roho Mtakatifu katika maisha yangu. Kwa kushirikiana na kumtegemea Yeye, natii amri yake ya "kujitwika utu mpya" (Warumi 6:1-4; Waefeso 4:24).

c. Sasa nampokea kwa dhati Yesu Kristo kama ukombozi wangu kutoka kwa Shetani na nachukua nafasi pamoja naye katika mahali patakatifu, nikimuomba Roho Mtakatifu atimilize kazi ya kupaa kwa Yesu kurudi mbinguni. Katika Jina lake najisalimisha kwa Mungu na kusimama dhidi ya ushawishi na hila za Shetani. Kwa kushirikiana na kumtegemea Mungu, natii amri yake ya "kumpinga ibilisi" (Waefeso 1:20- 23; 2:5; 4:27; 6:10-18; Wakolosai 1:13; Yakobo 4:7; 1 Petro 3:22; 5:89).

d. Sasa nampokea kwa dhati Roho Mtakatifu kama upako wangu katika kila nyanja ya maisha yangu ya kila siku. Nayafungua kabisa maisha yangu kwake kunijaza upya katika utii wa agizo kuwa "mjazwe na Roho Mtakatifu" (Waefeso 5:18; Yohana 7:37-39; 14:16,17; 15:26,27; 16:7-15; Matendo 1:8).

"Baada ya kufanya ukiri na maamuzi haya ya imani, sasa napokea ahadi za Mungu kwangu kwa siku ya leo (Waebrania 4:1-13). Kwa hiyo, najiburudisha katika tumaini la imani, nikitambua kuwa wakati wa majaribu na mahitaji, BWANA mwenyewe atahusika na kunitia nguvu na kuwa utoshelevu wangu. (1 Wakorintho 0:13)."

Maombi ya Vita

Nashauri usome (uombe) maombi haya kwa dhati na kwa sauti kama maombi yako kwa BWANA. Naamini, baadaye utaweza kufanya maombi haya, hasa kwa kutumia ukweli wa mafundisho yaliyoainishwa katika maombi haya, katika maombi yako ya kila siku bila ulazima wa kuyasoma.

Shetani anachukia sana maombi. Nashauri pia kwa wale wanaohusika na huduma ya Maombi na Maombezi (hasa maombezi ya ukombozi kwa watu waliofungwa na nguvu za mapepo, majini na mizimu), ni vyema wakasoma (wakaomba) maombi haya kwa pamoja kwa sauti kabla ya kuanza kumwombea mtu husika.

Ni ukweli wa Mungu kuwa Shetani hawezi kushindana na anapigana kwa nguvu zake zote kuhakikisha wakristo hawafanyi maombi. Wanaomaanisha katika maombi ya kivita wanapaswa kutumia maombi ya aina hii kumshambulia ibilisi.

MAOMBI

Baba yangu wa Mbinguni, nainama mbele zako katika kukuabudu na kukusifu. Najifunika kwa damu ya BWANA wetu Yesu Kristo kama ulinzi wangu wakati ya maombi haya. Najisalimisha kabisa na bila kinyongo, katika kila eneo la maisha yangu, kwako BWANA. Nasimama dhidi ya kazi zote za Ibilisi Shetani ambazo zingenizuia wakati huu wa maombi, na najielekeza kwa Mungu wa kweli aishiye na nakataa kuwa shirika na Shetani kwa jambo lolote wakati wa maombi haya.

[Shetani, nakuamuru, katika Jina la BWANA wetu Yesu Kristo, ondoka katika uwepo wangu ukiwa pamoja na mapepo yako, na naimwaga damu ya Yesu Kristo ifanye mpaka kati yangu na wewe]

Baba yangu wa Mbinguni, nakuabudu na kukuinulia sifa. Natambua kwamba Wewe unastahili utukufu wote, heshima na sifa. Narejea utii wangu kamili kwako na kuomba kwamba Roho Mtakatifu aniwezeshe katika maombi haya.

Nakushukuru BABA yangu wa Mbinguni, kwamba umenipenda hata kabla ya misingi ya ulimwengu haijawekwa, na kwamba ulimtuma BWANA wetu Yesu Kristo duniani afe kwa ajili yangu ili niweze kukombolewa. Nakushukuru kwa sababu Yesu Kristo alikuja kama mwakilishi wangu, na kupitia Yeye umenisamehe kabisa dhambi zangu zote; umenipa uzima wa milele; umenipa haki kamili ya Yesu Kristo BWANA wangu kwa hiyo nahesabiwa haki. Nakushukuru kwamba ndani yako umenikamilisha, na umejitoa kwangu kama msaada wangu na nguvu yangu

ya kila siku.

Baba yangu wa Mbinguni, nifungue macho yangu ili nione namna ulivyo mkuu na namna baraka zako kwangu zilivyo kamili kwa siku ya leo. Kwa Jina la Yesu Kristo nachukua nafasi yangu mahali patakatifu katika ulimwengu wa roho nilipoketishwa pamoja na Kristo nikikemea falme na mamlaka, wakuu wa giza, majeshi ya mapepo wabaya katika ulimwengu wa roho na kuwaweka chini ya miguu yangu.

Nashukuru kwa ushindi wa Yesu Kristo alioshinda kwa ajili yangu Msalabani na kufufuka kwake na hivyo nimeketishwa pamoja na BWANA wetu Yesu Kristo mahali patakatifu katika ulimwengu wa roho. Kwa hiyo, naamuru hizo falme na mamlaka na roho zote za giza zijisalimishe kwangu katika Jina la Yesu Kristo.

Nashukuru kwa silaha ulizonipa na hivyo navaa mshipi wa ukweli, dirii ya haki, viatu vya amani na chapeo ya wokovu. Nainua ngao ya imani juu ya mishale ya moto ya adui, na kuchukua katika mkono wangu upanga wa roho, Neno la Mungu, na kutumia Neno la Mungu dhidi ya nguvu zote za uovu katika maisha yangu, na kuvaa silaha hizi na kuishi nikikutegemea kabisa Wewe, Roho Mtakatifu.

Nakushukuru Baba yangu wa Mbinguni, kwamba BWANA wetu Yesu Kristo aliharibu enzi zote na mamlaka na kuzifanya si kitu hadharani na kupata ushindi juu yao ndani yake. Ninadai ushindi wote huo kwa ajili ya maisha yangu leo. Nakataa katika maisha yangu mashitaka yote, shutuma, na majaribu ya Shetani.

Nathibitisha kwamba Neno la Mungu ni kweli, na mimi naamua kuishi leo katika mwanga wa Neno la Mungu. Nachagua, Baba wa Mbinguni, kuishi katika kukutii Wewe na katika ushirika nawe. Fungua macho yangu na kunionyesha maeneo ya maisha yangu ambayo hayakupendezi. Tengeneza maisha yangu ili kusiwepo na mwanya wa kumfanya Shetani aweke makao ndani yangu.

Nionyeshe sehemu yoyote yenye udhaifu katika maisha yangu. Nionyeshe sehemu yoyote ya maisha yangu ambayo ninapaswa kuikabili kwa maana ya kuifanyia marekebisho ili nikupendeze Wewe. Kila siku nasimama ili nikupendeze na kuifanya ile huduma ya Roho Mtakatifu katika maisha yangu.

Kwa imani na katika kukutegemea Wewe, najivua utu wa kale na kusimama kwenye ushindi kupitia msalaba ambapo BWANA wetu Yesu Kristo aliachilia

utakaso wa utu wangu wa kale. Nauvaa utu mpya na kusimama kwenye ushindi kupitia ufufuo wa Yesu Kristo na yote aliyonikirimia ili niweze kuishi kwa ushindi dhidi ya dhambi.

Kwa sababu hiyo, leo najivua utu wangu wa zamani ulio na ubinafsi na kuuvaa utu mpya wenye upendo. Nauvua utu wa kale uliojaa hofu na kuuvaa utu mpya uliojaa ujasiri wa Mungu. Nauvua utu wa zamani ulio na udhaifu na kuuvaa utu mpya uliojaa nguvu. Leo nauvua utu wa zamani uliojaa tamaa za udanganyifu na kuuvaa utu mpya uliojaa haki na usafi.

Kwa njia yoyote ile, nasimama katika ushindi wa kupaa na utukufu wa Mwana wa Mungu ambapo enzi yote na mamlaka vilitiishwa kwake, na mimi nadai nafasi yangu katika ushindi wa Kristo dhidi ya maadui wote wa roho yangu. Roho Mtakatifu, naomba unijaze. Njoo katika maisha yangu, kuvunja kila sanamu na kuondoa kila aina ya adui aliyejificha ndani yangu.

Nakushukuru Baba yangu wa Mbinguni, kwa kuonyesha mapenzi Yako kwangu kila siku kama ulivyoyadhihirisha kupitia Neno lako. Kwa hiyo, nadai mapenzi yote ya Mungu juu yangu siku ya leo yaweze kutimizwa.

Nakushukuru kwamba umenibariki na baraka zote za rohoni katika ulimwengu wa roho kupitia Yesu Kristo. Nakushukuru kwa sababu umenizaa kupitia tumaini lililo hai kwa ufufuko wa Yesu Kristo kutoka katika wafu. Nakushukuru kwa sababu leo umenikirimia uwezo wa kuishi nikiwa nimejazwa na Roho Mtakatifu kwa upendo na furaha na uwezo wa kujidhibiti. Natambua haya ni mapenzi Yako kwangu na kwa sababu hiyo nakataa juhudi zote za Shetani, mapepo, majini, mizimu na nguvu zote za giza kuninyang'anya yale mapenzi Yako kwangu.

Leo nakataa kuamini hisia zangu na nang'ang'ania ngao ya imani dhidi ya mashtaka na madai yote ya Shetani ambayo anayapandikiza katika akili yangu. Nadai mapenzi makamilifu ya Mungu kwangu siku ya leo.

Kwa Jina la Yesu Kristo BWANA wetu, najisalimisha kabisa kwako eeh Mungu, Baba yangu wa Mbinguni, kama sadaka iliyo hai. Nachagua kutokujifananisha na watu wa dunia hii. Nachagua kugeuzwa kwa kufanywa upya nia yangu na naomba unionyeshe mapenzi yako na uniwezeshe kutembea katika utoshelevu wako wote siku ya leo.

Nakushukuru Baba yangu wa Mbinguni, kwamba silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome; zikiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu, na kuteka kila fikra iweze kumtii Bwana Yesu Kristo.

Kwa sababu hiyo, katika maisha yangu binafsi, leo naangusha ngome zote za Shetani na kubomoa mipango yake yote iliyopangwa dhidi yangu. Naangusha ngome zote za Shetani dhidi ya akili na mawazo yangu na kusalimisha akili yangu kwako, Roho Mtakatifu.

Nathibitisha, Baba yangu wa Mbinguni, kwamba haukutupatia roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi. Hivyo, navunja na kuangusha ngome za Shetani dhidi ya hisia zangu leo, na naachilia hisia zangu kwako. Nabomoa ngome za Shetani zilizojiinua kinyume na matakwa yangu leo, nakabidhi mapenzi yangu yote kwako, na nachagua kufanya maamuzi sahihi ya imani. Nabomoa ngome za Shetani zilizojiinua dhidi ya mwili wangu leo, na nautoa tena mwili wangu kwako, nikitambua kwamba mimi ni hekalu yako; na nafurahia rehema yako na wema wako kwangu.

Baba yangu wa Mbinguni, naomba siku nzima ya leo unihuishe; nionyeshe njia Shetani anayotumia kunizuia na kunijaribu na kunidanganya na kunibadilishia ukweli na kunipotosha. Niwezeshe kuwa mtu nitakayekupendeza siku zote. Niwezeshe niwe shujaa wa maombi. Niwezeshe niwe shujaa kiakili na nifikiri mawazo yako, na kukupa nafasi inayostahili katika maisha yangu.

Kwa mara nyingine tena, najifunika kwa damu ya Bwana Wetu Yesu Kristo na nakuomba Roho Mtakatifu ulete ndani yangu kazi yote ya msalaba, kazi yote ya ufufuo, kazi yote ya utukufu, na kazi yote ya Pentekoste katika maisha yangu leo. Najisalimisha kwako.

Nakataa kukatishwa tamaa. Wewe ni Mungu wa matumaini yote. Umethibitisha nguvu yako kwa kumfufua Yesu kutoka wafu, na mimi nadai ushindi wako dhidi ya nguvu zote za kishetani katika maisha yangu, na nakataa vikosi vyote vya nguvu za giza.

Naomba yote haya katika Jina la Bwana Yesu Kristo kwa moyo wa shukrani. Amina.

JINA NA DAMU YA YESU KAMA SILAHA YA VITA

Naiachilia damu ya Yesu kwenye maisha yangu
Naitamka damu ya Yesu kwenye maisha yangu
Ile damu ikawe ushindi wangu
Kwenye vita vikali naitanguliza damu ya Yesu
Kwenye mstari wa mbele wa jeshi, la vita vikali
Naitanguliza damu ya Yesu
Ikaharibu kabisa nguvu ya adui
Na mamlaka yake
Ikaharibu kabisa nguvu ya adui
Na uweza wake

Ile damu ikanifiche
Dhidi ya mashambulizi ya yule adui
Ile damu ikanitenge
Na visasi vyote vya yule adui
Ile damu ikaniondolee hatia, hukumu, mashtaka na uovu wote
Mbele zako eeh BWANA

Hati ya mashitaka ikafutwe
Kwa damu ya Yesu
Hati ya hukumu ikafutwe
Kwa damu ya Yesu
Kile kiambaza cha dhambi
Kinachonitenga na Mungu aliye hai
Kikavunjwe kwa damu ya Yesu

Nikastahili katika hali ya kutokustahili
Hiyo damu ya Yesu inipe haki
Hiyo damu ya Yesu inistahilishe
Hiyo damu ya Yesu inipe neema ya ushindi

Kwa damu ya Yesu
Kila madhabahu iliyojengwa juu yangu

Katika ulimwengu wa roho
Hiyo madhabahu ya giza inayonifuatilia
Kwenye maisha yangu
Leo naivunja
Haijalishi hiyo madhabahu imejengwa na wachawi, mizimu, waganga
Na kila aina ya nguvu za giza
Leo naivunja kwa damu ya Yesu

Kwa damu ya Yesu
Kila madhabahu ya giza
Inayonifuatilia kwenye eneo langu la kazi, biashara, uchumi, ndoa, familia, afya, elimu
Na kila eneo katika maisha yangu
Hiyo madhabahu inayonizuia
Leo naivunja kwa damu ya Yesu
Naifikisha mwisho hiyo madhabahu ya giza ambayo ni kikwazo kwenye maisha yangu
Kwa Jina la Yesu
Kwa mamlaka iliyo ndani yangu
Leo hii ninafuta maneno yote yaliyotamkwa dhidi yangu
Kwenye hiyo madhabahu ya giza
Leo nafuta hayo maneno
Kwa Jina la Yesu

Maneno yote yaliyotamkwa kinyume changu
Nayaondoa leo
Kwa Jina la Yesu

Ile madhabahu iliyotamka umasikini, magonjwa, laana, mikosi na roho ya kutofanikiwa,
Ile madhabahu iliyotamka kushindwa kwenye mipango yote, mauti kwenye maisha yangu
Nayafuta hayo matamko yote kwa damu ya Yesu

Kwa Jina la Yesu
Sasa yale mabaya yote waliyonitamkia
Nayarudisha kwao
Wametamka mauti narudisha kwao

Wametamka laana narudisha kwao
Wametamka magonjwa narudisha kwao
Wametamka umasikini narudisha kwao
Wametamka kuharibikiwa kwa kila jambo nilifanyalo narudisha kwao
Wametamka kushindwa na kutoendelea narudisha kwao
Wametamka ajali narudisha kwao
Yale mashimo waliyonichimbia nawaingiza wao
Ile mitego waliyonitegea wakanaswe wao wenyewe
Kwa Jina la Yesu Kristo

Kwa Jina la Yesu
Leo naondoa mipaka yote
Niliyowekewa kwenye maisha yangu
Ile mipaka inayonizuia kwenda mbele na kuniwekea mipaka katika mwendo wangu
Leo hii naifuta mipaka ya kichawi, mizimu, mapepo na majini
Mimi sitawekewa mipaka na ile marufuku yao naiondoa
Kwa damu ya Yesu

Mimi sitawekewa mipaka
Mipaka yote naifuta
Ile marufuku yenu leo naiondoa
Marufuku ya kutofanikiwa
Marufuku ya kutokubarikiwa
Marufuku ya kutokuoa au kutokuolewa
Marufuku ya kila aina mliyoiweka katika maisha yangu
Naiondoa leo
Kwa damu ya Yesu

Mliweka marufuku kwa Daniel
Akaipangua hiyo marufuku kwa kuomba kila siku mara tatu
Na mimi leo naipangua marufuku yote mliyoniwekea kwa Jina la Yesu

Kwa Jina la Yesu
Kama ilivyoandikwa katika Isaya 54:15-17
Nimemuumba mtu atengenezaye silaha
Lakini pia nimemuumba muharibu silaha
Mimi ndiye muharibu silaha

Na leo naziharibu silaha zote za nguvu za giza zilizotengenezwa dhidi yangu
Hizo silaha naziharibu
Iwe silaha ya magonjwa, mauti, ajali, misiba
Hizo silaha naziharibu kwa damu ya Yesu

Kwa Jina la Yesu
Ewe nafsi yangu uliyewekwa kwenye vifungo vya giza
Leo ninakuondoa
Naitenganisha nafsi yangu na madhabahu za mizimu
Naitenganisha nafsi yangu na madhabahu za kichawi
Naitenganisha nafsi yangu na madhabahu za uganga
Naitenganisha nafsi yangu na madhabahu za kuzimu
Ewe nafsi yangu toka kuzimu
Ewe nafsi yangu toka kwa wachawi
Toka kwenye mizimu
Toka kwenye uganga

Kwa Jina la Yesu
Leo hii najiondoa mwenyewe kokote ulikoniita
Iwe ni makaburini, kwenye miti, kwenye bahari, kwenye mashimo, kwenye milima
Iwe kwenye mapango, majabali, miamba, vyoo, majalala, mitaro
Najiondoa leo
Kwa damu ya Yesu

Kwa Jina la Yesu
Sasa ninaiondoa kazi yangu iliyowekwa kwenye mashimo na makaburi
Naiondoa elimu yangu, ndoa yangu, biashara yangu, mume wangu (au mke wangu),
Naondoa huduma yangu. Haitawekwa kwenye makaburi
Biashara zangu, baraka zangu, kazi yangu, haitawekwa kwenye makaburi
Chochote kile mlichoweka kwenye makaburi, mapango, bahari, majabali
Leo naondoa
Hatma yangu hamtaizika kama hatma ya Yusufu ilivyojaribu kuwekwa katika shimo
Leo naiondoa mlikoizika
Kwa Jina la Yesu

Katika Jina la Yesu

Natangaza urejesho wa ndoa yangu
Natangaza urejesho wa kazi yangu
Natangaza urejesho wa baraka zangu
Natangaza urejesho wa afya yangu
Natangaza urejesho wa elimu yangu
Natangaza urejesho wa biashara yangu
Natangaza urejesho wa karama, wito, vipawa na huduma yangu
Natangaza urejesho wa nguvu za kiungu, usomaji na kulitafakari Neno la Mungu na kuomba
Katika Jina la Yesu

Kwa Jina la Yesu
Kila kifungo, kila minyororo iliyofungwa kwenye maisha yangu
Leo naikata kwa Jina la Yesu
Samson akafungwa kamba ili apelekwe kwa Wafilisti wakamtese
Lakini akazikata hizo kamba
Yamkini nimefungwa kamba
Ili nipelekwe kwa watesaji
Leo nakata hizo kamba
Kamba ya mateso leo naikata
Kamba ya magonjwa leo naikata
Kamba ya mauti leo naikata
Kamba ya mikosi leo naikata
Kamba ya laana leo naikata
Kamba ya kushindwa leo naikata
Kwa Jina la Yesu

Nakata hizo kamba katika mikono yangu, miguu yangu, shingo yangu,
Nakata hizo kamba kwenye ufahamu wangu,
Nakata hizo kamba kwenye akili yangu
Nakata hizo kamba walizofunga kwenye mwili wangu wote
Katika Jina la Yesu

Kwa Jina la Yesu
Sasa niko huru
Kama vile Yesu alivyomfufua Lazaro
Akasema mfungueni mwacheni aende zake
Na mimi niko tayari

Kwenda mashariki, magharibi, kaskazini na kusini
Hakuna kinachonizuia kupata baraka zangu alizoniahidia BWANA
Kwa damu ya Yesu

Sasa ninapiga walinzi wote wa kipepo waliowekwa kuratibu nyendo zangu
Kwenye gereza la magonjwa, umaskini, laana, mauti
Ninyi walinzi mliopewa kazi ya kuniratibu ili nisipate kazi, nisifanikiwe
Enyi walinzi, leo hii nawashughulikia kama vile Paulo na Sila
Walivyosifu na kuabudu pale gerezani
Hata milango ya gereza ikafunguka

Kama vile Petro alivyowekwa kwenye chumba cha ndani
Akatokea malaika akampiga kwenye ubavu
Ile minyororo ikamwacha
Na vile vikosi vya askari vikashindwa kumkamata Petro
Na yale malango yakafunguka
Ndivyo hivyo leo enyi walinzi
Leo nawapiga kwa Jina la Yesu
Nawakumbusha mlilinda kaburi la Yesu
Ili asitoke
Lakini siku tatu zilipotimia lile kaburi likawa wazi na Yesu akatoka
Na ninyi walinzi mkawa kama wafu
Ndivyo ninavyowafanya mkawe kama wafu
Kwa damu ya Yesu

Kwa Jina la Yesu
Mwili wangu ni hekalu la Roho Mtakatifu
Siyo nyumba ya mapepo, wala majini, wala siyo kiti cha majini
Hivyo nyie majini, mapepo na mizimu mliokaa kwenye mwili wangu
Iwe kwa sababu yoyote au madai yoyote
Leo hii nabatilisha madai yenu
Nabatilisha sababu zenu
Kwa damu ya Yesu

Hata kama mna madai na mna sababu
Hizo sababu na madai ni batili
Kwa damu ya Yesu
Hivyo siwasikilizi maana shauri lenu limetupiliwa mbali

Mashitaka yenu yametupiliwa mbali

Ninalo neno moja juu yenu ninyi mapepo, majini na mizimu
Nimepewa amri ya kutoa pepo
Na sasa ninawatoa
Iwe majini, mapepo, mizimu, uchawi, uganga
Nawaondoa kwa damu ya Yesu
Mahali popote mlipo katika mwili wangu
Makazi yenu yote katika mwili wangu ni batili
Nawaondoa kwa Jina la Yesu

Mizimu ya ukoo mliofunga mambo yangu yote
Leo nawaondoa katika maisha yangu na familia yangu
Katika Jina la Yesu
Natangaza rasmi leo kwamba ile mizimu ya ukoo na asili yangu
Haitanifuatilia kwenye maisha yangu kwa sababu mimi ni kiumbe kipya katika Kristo Yesu
Nimeoshwa na kusafishwa kwa damu ya Yesu
Natangaza uhuru na uzima katika Jina la Yesu
Natangaza kufunguliwa
Natangaza mwendo mpya pamoja na Yesu Kristo BWANA wangu
Ushindi ni sehemu ya maisha yangu
Kwa damu ya Yesu

Nimeomba kwa imani na imekuwa hivyo
Katika Jina la Yesu Kristo Mwana wa Mungu aliye hai

Amina.

MAOMBI YA SIFA KWA MUNGU

Una roho ya kukata tamaa? Naam, Isaya 61:3 inaelezea kuhusu "vazi la sifa" kwa ajili ya hali yako. Kama una matatizo ya kuvaa vazi hilo la sifa siku ya leo, maneno haya yatakufanya uyatafakari majina na sifa za Muumba wako. Mungu wetu ni mtakatifu, mwenye upendo, wa milele na wa ajabu zaidi ya ufahamu wetu. Hebu tuombe maneno haya kwa pamoja na tuyaondoe macho yetu mbali na matatizo yetu ya kidunia na tujielekeze kwa Baba yetu wa mbinguni ambaye anastahili sifa zetu!

Abba, Baba yangu, wewe ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho. Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai. Wewe ni Muumba wangu na Mshauri wangu, ukiniongoza kila siku kufanya maamuzi yenye hekima. Wewe ni mfariji wangu wakati wa huzuni, maumivu, au dhiki. Ninakusifu na kukushukuru kwa kujongea karibu yangu pale ninapojongea karibu yako. Wewe ni El Roi, Mungu Unionaye, nawe ni wa milele, Bwana. Wewe ni Baba yangu aliye mbinguni, na Baba wa yatima. Ni jinsi gani ulivyo Mkuu na uaminifu wako, Mungu, kila siku.

Wewe ni Mtakatifu, lakini ulifanya njia kwa ajili yangu kukukaribia. Ninakushukuru kwa kuwa Msaidizi wangu, na kwa ajili ya Roho Mtakatifu ashuhudiaye moyoni mwangu, kunirekebisha, na kuwa mlinzi wa maisha yangu. Wewe huonekani, lakini nakuona kwa macho ya imani. Wewe ni Yehova Mungu, na Yehova Yire, Yeye atoaye kwa ajili ya mahitaji yangu yote. Ninakushukuru Yehova Rafa, Mungu wangu aniponyaye, na kwa kuwa Yehova Rah, Mchungaji wangu mwaminifu. Wewe si tu Mfalme, lakini wewe ni Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana. Na ndiyo, wewe ni Yesu, jina lipitalo majina yote.

Kwa moyo wangu wote ninakushukuru Mungu. Wewe ndiye Mesiya, Mfalme ajaye karibuni. Wewe unaelewa yote, una ujuzi wa mambo yote. Wewe uko kila mahali; mahali pote wakati wote. Wewe ni amani yangu, Mlinzi wangu, na Kuhani Mkuu ambaye alikuwa Mkombozi wangu na dhabihu yangu ya milele. Ulikufa ili unikomboe; Ulifufuka tena na kunipa ushindi dhidi ya kifo. Mimi si mtumwa tena wa dhambi; wewe ni Wokovu wangu, Mkombozi wangu na Kimbilio langu. Unanipa tumaini jipya ndani yangu.

Ninakusifu kwa sababu wewe ni Amini na Kweli. Wewe ni Mwalimu wangu, na uelewa wako na hekima yako ni zaidi ya akili za kibinadamu; umeniahidi hekima ninapokuomba. Wewe ni Njia, Kweli, na Uzima. Bwana, napenda ulivyo na furaha kwa ajili yangu na kwamba wanifurahia kwa kuimba. Unajua idadi ya nywele katika kichwa changu, na waniwazia yaliyo mema kila wakati.

Unaniandalia mahali ili siku moja niishi nawe milele. Labda wakati huo ndipo nitaweza kukusifu kiuhalisia kwa namna ambayo haiwezekani kukusifu nikiwa hapa duniani; kwa namna ambayo kweli unastahili kuabudiwa.

Upendo wangu wote, sifa zangu zote nakupa wewe. Bwana, eeh, Bwana. Ni namna gani Jina lako lilivyotukuka. Nakusifu, nakuabudu nakusujudu.

Amina.

MAOMBI YA MSAMAHA NA UREJESHO

Je umeanguka katika tabia hatari ambazo zinakwaza imani yako na ushuhuda wako? Wote tumekuwa katika hali hiyo kwa wakati fulani. Kama hatia na aibu zimeweka doa katika maisha yako, na majuto yanajaza nafasi zilizoachwa wazi kwenye historia yako, jipe moyo. Mungu anatoa upendo, msamaha, na urejesho. Kama hali hii inakuhusu wewe, hapa chini kuna sala ya toba na urejesho itakayokusaidia kukurejeshea upya furaha, matumaini, na maisha.

Bwana Yesu, nimechoka na maisha ya kushindana na dhambi. Najisikia kuwa mbali nawe. Chaguzi zangu hazikuniongoza kuwa katika maeneo sahihi ya maisha. Nimesikiliza minong'ono ya adui zangu badala ya Maneno yako katika Maandiko Matakatifu, na matokeo yake yamekuwa mabaya kwangu.

Zamani nilitembea nawe, moyo wangu ulitamani uongozi wako. Hata hivyo, kidogo kidogo, nilibadilisha ukweli wako na kuanza kuishi maisha ya majaribu na udanganyifu ambayo yalinipeleka mbali nawe. Badala ya kuyateka nyara mawazo yote ya uovu na kutubu mara moja, niliyaruhusu kukua na hatimaye kushindwa kujidhibiti. Toba haikuwa moja ya misamiati yangu. Lawama, udanganyifu, au kujaribu kujifariji kwa dhambi nilizokuwa natenda havikunisaidia. Vyote vilinifanya nizame zaidi katika dhambi.

Umeniumba kwa mfano wako mwenyewe, Bwana. Unajua mawazo yangu kabla sijatamka. Umeuchunguza moyo wangu na kuziona njia zangu na nia yangu. Roho wako alinionya, lakini nilipuuza. Kukata tamaa na kuvunjika moyo vimeathiri maisha yangu.

Hivyo, leo nakiri kuwa nakuhitaji sana BWANA wangu. Umeahidi kwamba kama tukikiri na kutubu dhambi zetu, Utatusamehe na kutufanya safi tena. Bwana, nahitaji sana msamaha wako. Toba iko katika moyo wangu na midomo yangu. Nataka kugeuka na kuwa na mwelekeo mpya – wa kurejea kwako Bwana. Lakini nahitaji msaada wako.

Kama vile ulivyoumba ulimwengu kutoka katika utupu, BWANA niumbie moyo safi nje katika utupu wangu. Ulilipia dhambi zangu kwa kifo chako mwenyewe.

Rejesha maisha yangu na ushirika ambao awali tulikuwa nao. Naelewa haunihukumu, hauwezi kunikana; Mimi ni mtoto wako milele. Lakini nachukua lawama zote, nakiri dhambi zangu zote. Mimi ndiye niliyevunja agano nawe na nimeangamia kwa namna nilivyokutenda dhambi.

Bwana, ondoa mizizi yote ya giza na angazia maisha yangu na uwepo wako Mtakatifu. Nisaidie kuelewa yote yaliyonifanya niende kinyume nawe. Nionyeshe chanzo cha uharibifu wangu. Je, ni kitu gani nilichoruhusu kuwa muhimu zaidi kuliko kukupenda na kukuheshimu Wewe? Kwa nini nilitafuta kutoshelezwa na watu au vitu vingine badala ya Wewe kuwa utoshelevu wangu? Wewe ndiye unipaye mahitaji yangu yote. Waijaza roho yangu kwa furaha ya kweli na amani zaidi ninavyoweza kuelewa.

Bwana, naomba urejesho wako uambatane na kuniwekea mipaka mipya kuzunguka maisha yangu. Siwezi kuchezea dhambi bila kuumizwa. Katika kunirejesha, nifundishe namna ya kusema hapana tena kwa mambo ambayo yanaweza kunidhuru na kuharibu ushuhuda wangu. Kama matendo yangu yamekwaza wengine, nionyeshe wapi na kwa nani nahitaji kuomba msamaha au jinsi ya kufanya marekebisho. Nisaidie kuzingirwa na watu watakaonitia moyo katika kuishi maisha ya utakatifu na watakaoniwajibisha na kuniambia ukweli kwa upendo. Kweli, aibu inayeyuka mbali na tunaponywa tunapokiri na kutubu mbele ya wengine na kuomba msaada wao.

Naelewa kwamba toba yangu haitaondoa madhara ya dhambi zangu. Nikitambua kwamba hautudhihaki kwa dhambi zetu na wala hauzikumbuki tena, na kwamba unaziweka mbali sawa na mashariki ilivyo mbali na magharibi, vyanifanya nijinyenyekeze kwako kwa mshangao mkubwa na shukrani nyingi. Hakuna matokeo machungu zaidi ya kutambua namna dhambi zangu zilivyokuumiza, au jinsi ulivyosulubiwa kwa ajili ya upendo wako kwangu. Kifo chako cha kusulubiwa msalabani kimenipa uzima wa milele pamoja nawe. Bwana, umeweka neema karibu na majuto yangu na kunipa matumaini mapya ya baadaye.

Asante BWANA Yesu, kwamba dhambi zangu hazikubatilisha uhusiano wangu nawe. Badala yake, kama mwanariadha aangukaye lakini anasimama tena na kuendelea na mbio, nami pia, niko tayari kuanza tena na kumaliza mbio ulizoweka kwa ajili yangu.

Kwa urejesho wako, BWANA Yesu, labda naweza kuwasaidia wengine kuelewa njia

ya kurejea kwako tena. Sitampa adui yangu ushindi tena. Badala yake, nitakubali ushindi wako. Badala ya kunyong'onyea, kwa msaada wako nitamruhusu Roho Mtakatifu kunipa moyo unaokutafuta wewe, ulio na shauku ya kuishi kwa ajili yako kwa maisha yangu yote. Asante Yesu kwa msamaha wako mtamu na ahadi ya urejesho.

Je, hujawahi kuomba maombi ya toba? Basi omba maombi haya kwa ajili ya msamaha wa dhambi na kupata wokovu.

BWANA Yesu, nakubali kwamba mimi ni mwenye dhambi. Nahitaji na ninataka msamaha wako. Nakubali kifo chako kama adhabu kwa ajili ya dhambi zangu, na natambua kwamba rehema na neema yako ni zawadi unayotoa kwangu kwa sababu ya upendo wako mkubwa, si kutokana na kitu chochote nilichofanya. Nisafishe na kunifanya kuwa mwanao. Kwa imani nakupokea ndani ya moyo wangu kama Mwana wa Mungu na kama Mwokozi na Bwana wa maisha yangu. Kuanzia sasa, nisaidie kukuishia Wewe, na Wewe ukidhibiti maisha yangu.

Katika Jina lako takatifu la thamani,

Amina.

ZABURI 91 SALA YA ULINZI

Zaburi 91 ni Andiko kwa ajili ya ulinzi ambalo waumini wamelitumia kwa maelfu ya miaka wanapokabiliana na hatari. Kama ambavyo msimu wa taabu uko katikati yetu, sala ya Zaburi 91 ni faraja na yenye ufanisi mkubwa tunapoomba kwa dhati kutoka moyoni kwa wale wampendao Mungu na wana mahusiano naye.

Zaburi 91 yaweza kuwa Maandiko muhimu sana hasa kwa siku zilizo mbele yetu, Siku za Ufunuo. Ukweli kuhusu ulinzi wa kiungu ni muhimu sana hasa katika wakati tunapotarajia matukio mengi yaliyotabiriwa katika ulimwengu wa roho kuanza kutokea. Imani sio hatua ya mwisho, lakini majibu kwa hatua za kuchukua mwanzoni!

Kwa maana hiyo, waweza kuyafanya maandiko ya Zaburi 91 kuwa Maombi yako binafsi.

Tumia Maandiko ya Zaburi 91 na kuyafanya kuwa maombi yako binafsi kwa kubadilisha viwakilishi. Mungu analiangalia Neno lake ili aweze kulitimiza, hivyo maombi ya Zaburi 91 kwa kuweka maneno “Mimi” au “Sisi" yana nguvu sana. Kuomba kwa namna hii kunakuweka katikati kabisa ya ukweli huo na nguvu hizo.

Kama hujawahi kuomba kwa kutumia Maandiko, hii yaweza kuonekana kama siyo kitu cha kawaida. Hata hivyo, vumilia. Ni sala ya tangazo, tangazo la imani. Aina hii ya maombi ni tofauti na maombi ya dua au mahitaji. Huleta mtazamo mpya kabisa.

Kama ikiwezekana, kariri sala yako ili uweze kuwa nayo wakati wote (katika moyo wako) wakati utakapoihitaji zaidi.

Tafakari Zaburi 91

Bwana anaweza kuzungumza nawe kuhusu maana ya maneno fulani na kile anachotaka ukipate unaposoma Zaburi 91. Kwa mfano, kama neno "kudumu" limejitokeza kuwa muhimu kwako, basi unaweza kuomba kupitia Zaburi 91

kama ifuatavyo: Bwana, nimefanya uamuzi wa kukaa mahali pako pa siri, mahali pa siri pake Yeye Aliye Juu.

Nimeamua kuwa hii ndiyo haja ya moyo wangu, lakini nahitaji msaada wako kukaa thabiti na kudumu chini ya kivuli chako. Eeh Bwana, kwa uwezo wangu mwenyewe hii haiwezekani. Lakini, katika Wewe, Eeh Bwana, mambo yote yanawezekana.

Zaburi 91

1. Aketiye mahali pa siri pake Aliye juu
   Atakaa katika uvuli wake Mwenyezi.

2. Nitasema, Bwana ndiye kimbilio langu na ngome yangu,
   Mungu wangu nitakayemtumaini.

3. Maana Yeye atakuokoa na mtego wa mwindaji,
   Na katika tauni iharibuyo.

4. Kwa manyoya yake atakufunika,
   Chini ya mbawa zake utapata kimbilio;
   Uaminifu wake ni ngao na kigao.

5. Hutaogopa hofu ya usiku,
   Wala mshale urukao mchana,

6. Wala tauni ipitayo gizani,
   Wala uele uharibuo adhuhuri,

7. Ijapo watu elfu waanguka ubavuni pako.
   Naam, kumi elfu mkono wako wa kuume!
   Hata hivyo hautakukaribia wewe.

8. Ila kwa macho yako utatazama,
   Na kuyaona malipo ya wasio haki.

9. Kwa kuwa Wewe Bwana ndiwe kimbilio langu;
   Umemfanya Aliye juu kuwa makao yako.

10. Mabaya hayatakupata wewe,
Wala tauni haitaikaribia hema yako.

11. Kwa kuwa atakuagizia malaika zake
Wakulinde katika njia zako zote.

12. Mikononi mwao watakuchukua,
Usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.

13. Utawakanyaga simba na nyoka,
Mwana-simba na joka utawaseta kwa miguu.

14. Kwa kuwa amekaza kunipenda
Nitamwokoa; na kumweka palipo juu,
Kwa kuwa amenijua Jina langu.

15. Ataniita nami nitamwitikia;
Nitakuwa pamoja naye taabuni,
Nitamwokoa na kumtukuza;

16. Kwa siku nyingi nitamshibisha,
Nami nitamwonyesha wokovu wangu.

SALA YA SHUKRANI

Mungu wa baraka zote,
Chanzo cha maisha yote,
Mtoaji wa neema yote:

Tunakushukuru sana kwa zawadi ya maisha,
Kwa pumzi inayotupatia uhai,
Kwa ajili ya chakula katika dunia hii
Kinachotegemeza maisha,
Kwa upendo wa familia na marafiki
Ambao bila wao kusingekuwepo maisha.

Tunakushukuru sana kwa siri ya uumbaji wako,
Kwa uzuri,
kwa kile ambacho macho yetu yanaweza kuona,
Kwa ajili ya furaha
Kwa kile ambacho sikio laweza kusikia
Na kwa yale ambayo hatuyafahamu kama wanadamu,
Na ambayo hatuwezi kuyaona
Yaliyoujaza ulimwengu ambayo ni ya ajabu
Kwa anga na mianga
Inayopeleka fikra zetu mbali zaidi
Na kutafakari ukuu wa uungu wako

Tunakushukuru sana kwa kutuweka katika jamii:
Kwa ajili ya familia ambazo zinatulea
Ili tuwe wenye msaada kwa jamii
Kwa marafiki wanaotupenda kwa uchaguzi wao binafsi,
Kwa marafiki kazini,
Waliotegemeza mizigo yetu na kazi za kila siku,
Kwa wale tusiowafahamu,
Wanaotukaribisha katika jamii zao na katika maisha yao,
Kwa ajili ya watu kutoka katika nchi nyingine
Ambao wanatusaidia kukua katika ufahamu,

Kwa watoto ambao wanajaza maisha yetu kwa furaha,
Kwa wale ambao hawajazaliwa,
Ambao ni sababu ya tumaini letu la baadaye.

Tunakushukuru sana kwa siku ya leo,
Kwa ajili ya uhai na siku moja zaidi ya kupenda,
Kwa fursa
Na siku moja zaidi ya kufanya kazi
kwa ajili ya haki na amani,
Kwa ajili ya majirani
Na mtu mmoja zaidi wa kumuonyesha upendo
Kwa neema yako
Na fursa nyingine ya kuwa uweponi mwako
Kwa ajili ya ahadi yako:
Ya kuwa pamoja na kati yetu
Kwa kuwa Mungu wetu,
Na kutupa wokovu wako.

Kwa ajili ya yote haya, na baraka zote,
Tunatoa shukrani zetu,
kwako Mungu wa milele, mwenye upendo,
Kwa njia ya Yesu Kristo tunaomba.

Amina.

MAOMBI YA KUMWABUDU NA KUMSUJUDU MUNGU (MUUMBAJI), YESU KRISTO (MWOKOZI), NA ROHO MTAKATIFU (MSAIDIZI)

Baba yetu mwenye wingi wa rehema, tunakubariki. Asante kwa kuwa Mfalme wa utukufu. Asante kwa kuwa Baba yetu, Mkombozi, Mchungaji na Mfalme. Asante kwa kutupatanisha tena nawe kupitia Mwana wako, Mwokozi wetu, Yesu Kristo. Tunakushukuru kwa sababu ya Roho Mtakatifu ambaye ni Wakili wetu uliyetuahidia anayetuwezesha kuwa mashahidi bora wa ufalme wako hapa duniani. Asante kwa kutupenda na kwa wakati wote kutuangalia. Bwana, acha tuwe ibada inayokupendeza wakati wote. Tutakusifu maadamu tunaishi. Tutaziimba sifa zako hata wakati tukipumua pumzi yetu ya mwisho kabla ya kufa. Tumaini letu ni kwako, BWANA Mungu wetu. Uliumba mbingu na nchi, bahari, na kila kitu ndani yake. Unatunza kila ahadi yako milele. Daima tunashangazwa na ukuu na utukufu wako.

Baba mwenye Utukufu wote, leo, tunakuheshimu na kukutukuza. Wewe ni Mungu wetu na tunasalimisha uaminifu na kuabudu kwetu kwako. Wewe ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho. Ulikuwepo kabla ya wakati na ukaumba kila kitu chenye uhai na kisicho na uhai. BWANA, ni Wewe pekee uliyeishika bahari katika vitanga vya mikono yako. Umeipima mbingu kwa vidole vyako na unatambua uzito wa dunia! Wewe ni wa ajabu kweli! Baba, kwako, mataifa yote ya dunia ni kama tone la maji ndani ya ndoo. Si kitu mbele yako zaidi ya vumbi katika mizani. Unainyanyua dunia yote kama vile punje ya mchanga! Bwana, wewe umeketi juu ya mviringo wa dunia, watu walioko duniani ni mfano wa nzige kwako. Umeitawanya mbingu na kuifanya kama pazia na hema yako.

Tunapoangalia juu angani, tunajua kwamba uliumba kila nyota tunayoiona. Wazionyesha kama jeshi, moja baada ya nyingine, ukiita kila moja kwa jina lake. Kwa sababu ya uweza wako mkuu na nguvu isiyolinganishwa, hata moja haipotei. Bwana, wewe ni Mungu wa milele, Muumba wa dunia yote. Kamwe hauna udhaifu wowote wala hauchoki. Hakuna awezaye kupima kina cha uelewa na ufahamu wako. Wewe ni mwema kwa kila mtu na unaachilia huruma juu ya

kila kiumbe ulichokiumba. Mfalme Mkuu, Wewe ni bendera yetu na ngao yetu, nguvu zetu na ulinzi wetu. Bwana Yesu, Wewe ni Mwokozi wetu, Mkombozi wetu na kupitia Wewe tumepewa haki. Roho Mtakatifu, Wewe ni Mtetezi wetu, Msaidizi wetu na chanzo cha nguvu zetu. Tunakupa sifa na kukuheshimu, katika ule Utatu Mtakatifu. HALLELUYA.

Baba wa utukufu, tafadhali masikio yako daima yasikie maombi yetu. Roho Mtakatifu, endelea kutufundisha jinsi ya kukupenda Wewe, Yesu, Baba yetu na Mungu wetu. Tafadhali gusa mioyo ya wale ambao hawamwabudu Bwana, na uwasaidie kumpenda Mungu kwa mioyo yao, roho, na nguvu. Tafadhali tukumbushe kila mmoja wetu mambo mengi ambayo Mungu anatufanyia kila siku na tusaidie kutumia muda mwingi zaidi katika kukusifu na kukuabudu. Tusaidie kuwa Kanisa linaloakisi utukufu wa Mungu kwa namna tunavyoishi maisha yetu. Roho Mtakatifu, tusaidie wakati wote kukumbuka kuhusu uwepo wako katika maisha yetu ya kila siku na tusaidie kuwa wepesi katika kutenda pale unapotutaka kuchukua hatua.

Baba unayesamehe, tusamehe dhambi zetu za kiburi, uasi, kutokutii, ubinafsi, chuki, na ibada ya sanamu. Bwana, tuondolee moyo wa kufanya ibada nusu. Utusamehe kwa kutokuliheshimu Jina lako na kukuchukulia kama siyo wa maana.

Samehe wote waliochagua kutokukuheshimu. Tusamehe ambao ni wazazi kwa kushindwa kuwafundisha watoto wetu kukuabudu. Bwana Yesu, samehe wale ambao wanachukua sadaka ya kifo chako kwa mzaha. Roho Mtakatifu, samehe wale ambao hawakutambui au Uwepo wako katika maisha yao ya kila siku. Bwana nisamehe kwa (orodhesha dhambi ambazo umetenda). Roho Mtakatifu, tukumbushe yote tunayopaswa kusamehe na tusaidie kuwa wepesi wa kusamehe. Kuhusu mimi, Roho Mtakatifu, nikumbushe wale ninaopaswa kuwasamehe. (Chukua muda na kumwomba Roho Mtakatifu kukuonyesha majina au sura za watu unaopaswa kuwasamehe. Kadri anavyokuonyesha, sema kwa sauti, "Nawasamehe ..... taja majina ya watu." Sasa, amini ya kwamba Bwana ataponya majeraha yote katika nafsi yako yaliyosababishwa na kutokusamehe.)

Roho Mtakatifu, utusaidie kutokushindwa na majaribu; lakini utuokoe na yule Mwovu.

Bwana Mungu Mwenyezi, Wewe watawala! Matendo yako ni makubwa na ya

ajabu namna gani! Njia zako Eee Mfalme wa mataifa yote, ni za haki na kweli. Ni nani asiyetetemeka mbele zako? Ni naye asiyelitukuza Jina Lako? Wewe peke yako ndiye Mtakatifu! Mataifa yote yatakuja na kuabudu mbele zako, kwa sababu matendo yako ya haki yameonekana na kudhihirishwa.

Katika Jina la Yesu, Amina.

ZABURI ZA KUSIMAMIA KATIKA MAOMBI

Zaburi zimekuwa chanzo cha msaada kwa Wakristo vizazi kwa vizazi. Katika maisha ya kiroho, Wakristo wamekuwa wakipitia katika hali mbalimbali; za mafanikio na za changamoto za maisha kama vile vita, njaa, magonjwa, misiba, dhiki, kukataliwa, n.k. Hata hivyo, katika hali zote bado tunatakiwa kuendelea kumtegemea Mungu, ambaye daima ni mtunza agano lake kwetu. Yeye anasema, "....kwa maana ninaliangalia neno langu, ili nilitimize" (Yeremia 1:12).

Kwa kuzingatia hilo, tumekuandalia Zaburi unazoweza kusoma (kama maombi) kwa kuzingatia maudhui unayotaka kuombea. Tuseme tu kwamba, Zaburi imesheheni maudhui mengi lakini hapa chini tumechambua maudhui machache tu kwa ajili ya kukusaidia unapoingia kwenye maombi.

NA.	MAUDHUI	SURA
1	Baraka	67, 72, 84, 128
2	Kumwita Mungu	4, 5, 22
3	Kujiamini	27, 36, 71, 125
4	Matendo ya Mungu	9, 18, 118
5	Mashaka	42, 73, 77
6	Uaminifu wa Mungu	105, 119:137-144, 146
7	Woga	37, 49, 91
8	Rehema	13, 28, 86
9	Amani	23, 133, 119:161-168
10	Nguvu ya Mungu	68, 93, 135
11	Sifa	65, 98, 138
12	Maombi	17, 20, 102
13	Ulinzi	59, 62, 124
14	Usalama wa Mungu	11, 16, 142, 46

15	Furaha	30, 47, 97
16	Haki	1, 15, 112
17	Wokovu	3, 14, 121
18	Dhambi na Toba	25, 32, 38, 51
19	Shukrani	75, 106, 136
20	Uaminifu	31, 40, 56
21	Ushindi	21, 76, 144
22	Hekima	90, 107, 111
23	Kuabudu	33, 34, 145

SHUKRANI

Tunamshukuru Mungu wa BWANA wetu Yesu Kristo kwa afya na uhai na kwa huduma aliyoweka ndani yetu kumtumikia. Kitabu hiki ni moja ya zao la ile huduma aliyotupa ya kumtumikia.

Tunaishukuru familia yetu yote kwa ujumla wake kwa malezi na ushauri. Watoto wetu Anna Grace, Gabriel Henry, Samuel Julius na Ezekiel Makene ambao wakati mwingine wanalazimika kukosa uwepo wetu tunapokuwa shambani mwa BWANA kumtumikia. Tunafurahi kwamba mnatambua umuhimu wa utumishi na mnatuchukulia katika hilo. Ni maombi yetu kwa Mungu aendelee kuwafunika kwa upendo wake na kuzikuza zile karama na vipawa vilivyo ndani yenu ili muweze kumtumikia Mungu pamoja na jamii kwa ujumla.

Wachungaji, Wazee wa Kanisa na familia nzima ya Kanisa la Faith Victory International ambayo imekuwa baraka sana kwetu. Tunathamini sana maombi yenu na namna ya ajabu mnavyotegemeza kazi ya BWANA. Mungu aendelee kuwatunza na akutane na mahitaji yenu ya kila siku.

Trevor Livingstone, umefanyika baraka sana katika kuandaa kazi hii. Umahiri wako katika ubunifu wa grafiti na upangaji wa kurasa umepelekea Kitabu hiki kuwa na taswira inayopendeza. Grafiti ulizotayarisha kwa ajili ya kukitangaza Kitabu hiki katika mitandao ya kijamii ilikuwa ya kiwango cha juu sana. Mungu aikuze karama yako na kipawa chako kwa ajili ya kumtumikia.

Elias Patrick, Mungu akubariki kwa huduma yako. Ubunifu wako katika mwonekano wa mbele na wa nyuma wa Kitabu umeendana na maudhui ya Kitabu hiki. Roho Mtakatifu aendelee kuachilia mafuta zaidi ndani yako ili ufikie utimilifu wa ile huduma aliyoiweka ndani yako.

Joseph Osilla, kwa ushauri na maelekezo yaliyowezesha kuboresha taswira ya Kitabu na hatimaye, kupitia Kampuni yako, kuchapisha Kitabu hiki. Mungu akubariki kwa sadaka uliyotoa kufanikisha kazi hii.

Na kwa wote mliofanikisha kazi hii na ambao mnaendelea kutuombea na kuitegemeza huduma ambayo Mungu ameiweka ndani yetu, Mungu awabariki sana.

> ***"Kukiwa bado ni mchana, tunapaswa kuendelea kuzifanya kazi zake Yeye aliyenituma. Usiku unakuja, na hakuna mtu atakayeweza kufanya kazi wakati wa usiku" (Yohana 9:4 TKU)***

@ Mch. Christine Mlingi na Mlingi Elisha Mkucha

DAUDI NA GOLIATI

Nguvu ya Ushindi Dhidi ya Majitu Katika Maisha Yako

Ni asili ya mwanadamu kujiepusha na changamoto za maisha na kupenda kufanikiwa bila kukutana na changamoto. Hata hivyo, kanuni ya Mungu ni kukufanikisha na kukuinua baada ya kupitia mitihani mikubwa na kushinda. Biblia imejaa mifano ya watu waliofanikiwa na kuinuliwa sana baada ya kushinda majitu katika maisha yao. Yesu mwenyewe alikirimiwa jina kuu kuliko majina yote na kuketishwa katika utukufu baada ya kushinda mateso ya msalaba, kaburi na mauti (Wafilipi 2 :8-11).

Ukweli ni kwamba ukubwa wa vita yako ndio utakaoakisi ukubwa wa kuinuliwa kwako. Huwezi kuwa na vita ndogo halafu utarajie kuinuliwa kwa kiwango kikubwa. Pamoja na kwamba Daudi alikwisha pakwa mafuta kuwa mfalme, alitakiwa kushindana na ufalme ili hatimaye akalie kiti cha kifalme. Hivyo, vita na hatimaye ushindi wa Daudi dhidi ya Goliati ndio uliosherehesha ufalme wake.

Kupitia Kitabu hiki, kinachochambua simulizi ya Biblia ya Daudi na Goliati, utajifunza namna ya kupambana na kushinda changamoto za maisha. Pamoja na kujenga tabia ya kusoma Biblia na kufanya maombi mara kwa mara, utapata *"Nguvu ya Ushindi Dhidi ya Majitu Katika Maisha Yako."*

Mchungaji Christine Mlingi **ni mhitimu wa Central Bible College, Dodoma, Tanzania. Ni Mwinjilisti ambaye shauku yake kubwa ni kuwafikia watu wengi kwa Neno la Mungu. Amehubiri ndani na nje ya Tanzania, mijini na vijijini na mahubiri yake yamekuwa yakifuatiliwa sehemu mbalimbali duniani kupitia mitandao ya kijamii.**

Mlingi Elisha Mkucha **[LL.B (UDSM); LL.M (NUS)] ni Wakili wa Kujitegemea; msomaji na mwanafuzi wa Biblia. Kwa sasa ni mwanafunzi wa Shahada ya Theolojia. Amewahi kufanya kazi Serikalini kwa zaidi ya miaka 18 na kuwa Mkurugenzi Mkuu wa moja ya mashirika makubwa yanayomilikiwa na Serikali.**

Mchungaji Christine na Mlingi ni Wachungaji waanzilishi wa Kanisa la Faith Victory International lililojengwa katika msingi wa Neno la Mungu; Maombi na Maombezi; Sifa na Kuabudu na Utoaji na lenye Kauli Mbiu ya *"Kumpenda Mungu na Kupendana Sisi kwa Sisi"* (Loving God, Loving Each Other).

Mchungaji Christine na Mlingi ni mke na mume na wamejaliwa watoto wanne, Anna Grace; Gabriel Henry; Samuel Julius na Ezekiel Makene. Wanaishi Dar es Salaam, Tanzania.